Nipashe
Alhamisi Aprili 23, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580213
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



TOLEO MAALUMU

## Subhash: Dk. Mengi alipigania uchumi wa viwanda nchini

UKURASA 3


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Wakala Misitu kuanzisha kiwanda mkaa mbadala
Wasomi: Silaha ya corona sasa ni mlo, usingizi kamili
Nguva ni binadamu au samaki?
AFYA
Hatua kubwa mkoa Kigoma kliniki ya mume, mke, mtoto
Hasa katika kipindi cha kwanza cha kliniki ya ujauzito, kuna mambo mengi ambayo wote wanapaswa kufahamu...

UKURASA 11

# JPM atoa maagizo mazito ya corona

• **Ataka** uchunguzi aliyeagiza Dar kunyunyiziwa dawa, atahadharisha matumizi barakoa za nje, aomba WB kusamehe madeni...wagonjwa wapya 30 wabainika... *Endelea ukurasa 2*



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Askofu Alex Malasusa wa KKKT Jimbo la Mashariki na Pwani (kushoto), Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Thaddeo Ruwaichi (wa pili kushoto), Mufti wa Tanzania, Abubakari Zubeir (wa tatu kushoto) katika maombi ya kukabiliana na tishio la ugonjwa wa COVID-19, kwenye viwanja vya ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

## Usajili mpya wanahabari wanukia

UKURASA 4


Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
GET IT ON Google Play
Download on the App Store

## Msako kuanza waliopandisha bei ya sukari

UKURASA 5



### BAA LA CORONA

**Epuka kusafiri maeneo tofauti kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa Covid – 19, hasa kwa watu wenye umri mkubwa au matatizo ya ugonjwa wa kisukari, moyo na mapafu. WHO**
- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**

MICHEZO MAXIME AZIHOFIA TIMU VIBONDE UK.23
MAONI, KATUNI UK.6

# Majaliwa aonya maambukizo Dar, wagonjwa wapya 30

**Na Romana Mallya**

IDADI ya watu waliopata maambukizo ya virusi vya corona nchini imefikia 284 baada ya wagonjwa wapya 30 kuthibitika kuwa na virusi hivyo ndani ya saa 24 kuanzia juzi.

Wakati hali ikiwa hivyo, serikali imewataka wakazi wa Dar es Salaam kuchukua tahadhari kwa kutozurura kutokana na jiji hilo kuwa na wagonjwa wengi.

Hadi Jumatatu jioni, serikali ilitangaza nchi kuwa kuwa na watu 254 waliokuwa wamepata maabukizo ya virusi hivyo baada ya wagonjwa wapya 84 kuthibitika kuwa navyo huku vifo vikiwa 10.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa maombi maalum kwa taifa dhidi ya virusi vya corona uliohusisha viongozi wa dini, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema hadi wakati huo idadi ya wagonjwa wapya ilikuwa 30.

"Hadi Aprili 21 (Jumanne), jumla ya wagonjwa 284 wamethibitika kuwa na corona, wagonjwa 256 wanaendelea vizuri, saba wako kwenye uangalizi wa karibu, 11 wamepona na idadi ya vifo Bara na Visiwani ni watu 10," alisema.

Waziri Mkuu alisema jumla ya watu 2,815 waliokuwa karibu na wagonjwa Bara na Visiwani wamefuatiliwa afya zao ambapo kati yao, 1,733 hawana maambukizo na wameruhusiwa kuungana na familia zao.

Alisema waliokutwa na virusi vya corona ni 12 ambao ni miongoni mwa watu 284 wanaoendelea kupatiwa huduma.

Majaliwa alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) liliikadiria Tanzania ifikapo mwishoni mwa mwezi huu, ingekuwa na wagonjwa 524,776 ambapo asilimia 80 wangekuwa na dalili nyepesi na asilimia 15 wangehitaji uangalizi maalum.

Waziri Mkuu alisema hadi siku hiyo, Tanzania haijafikia idadi hiyo ya wagonjwa ambayo WHO iliikadiria.

Alisema Jiji la Dar es Salaam na Zanzibar ndiyo maeneo yanayoongoza kwa kuwa na maambukizo makubwa kulinganisha na mikoa mingine.

"Serikali inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti kuenea zaidi kwa ugonjwa huu ikiwamo kutoa elimu ya namna ya kujikinga na kuna kamati za kitaifa kwa ngazi mbalimbali zenye lengo la kufuatilia hatua kwa hatua za kuchukua za hali ya ugonjwa na kutoa mapendekezo kwa serikali.

"Tumeunda kamati ya kitaifa inayohusisha mawaziri wa mabaraza ya mawaziri Bara na Visiwani ikiongozwa na Waziri Mkuu, tumeunda kamati ya makatibu wakuu Tanzania Bara na Visiwani ikiongozwa na makatibu wakuu viongozi, tumeunda timu ya madaktari waliobobea kwenye utafiti, tiba na watoa huduma," alisema.

Alisema kamati zote zina lengo la kufanya tathmini hatua kwa hatua na kila maambukizo yanayopatikana na zinaishauri serikali njia za kukabiliana nazo.

Vilevile, alisema wametoa maelekezo kwa kamati za ulinzi na usalama katika ngazi za mikoa na wilaya kuhakikisha wanashirikiana na kamati za maafa na kufuatilia ugonjwa ngazi zote.

United Republic of Tanzania
Ministry of Water

Enabel
Belgian Development Agency

**CALL FOR BIDS
(RE-ADVERTISED)**

**REHABILITATION OF MKONGORO GRAVITY-FED WATER SUPPLY SCHEME**

The Kingdom of Belgium through Enabel and the Government of Tanzania through the Ministry of Water, are implementing a water and sanitation project in Kigoma region. This is a 5-year project which runs through June 2022 and aims to promote provision of sustainable water supply services in the region. This intervention has three key result areas namely: 1) sustainable water supply operations and maintenance, 2) water supply scheme rehabilitation and extension and 3) promotion of safe hygiene practices in domestic water management. Under the second result area, the Water and Sanitation Kigoma Region Project (WASKIRP) is now inviting bids from qualified construction companies and consulting firms for the works program for the Mkongoro Gravity-fed water supply scheme.

**Rehabilitation Works**
This public works contract will consist of construction of a new intake, a treatment plant, transmission mains and distribution network which includes distribution points, in conformity with the conditions of the provided tender documents. The preferred contractor will have demonstrated financial and technical capacity to carry out the assignment described in the specifications of this tender.

**Duration:** 8 months with a post-construction defects liability period of 12 months.
**Location:** Mkongoro in Kigoma rural district in the region of Kigoma.

**More information and bid documents of these two assignments are available at: https://btctanzania.wordpress.com/**

**The works contract notice is also published on the Enabel website, www.enabel.be, in the Belgian Public Tender bulletin (BDA) and on the Organisation for Economic Cooperation and Development (OECD) website.**

215712002




Mafundi wakichimba kaburi sehemu atakayozikwa Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Mlima wa Moto, Dk Getrude Lwakatare, kanisani hapo Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. Maziko hayo yanatarajiwa kufanyika leo. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# JPM atoa maagizo mazito corona

**Na Romana Mallya**

WAKATI idadi ya watu walioambukizwa virusi vya corona nchini ikifika 284, Rais John Magufuli amevitaka vyombo vya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi wa vifaa vya kujikinga na maambukizo ya virusi hivyo vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi.

Kiongozi huyo wa nchi pia ameviagiza vyombo hivyo kufanya uchunguzi dhidi ya aliyeagiza Jiji la Dar es Salaam kupuliziwa dawa za kukinga ya maambukizo, akibainisha kuwa ni 'upuuzi mtupu' kwa kuwa virusi haviwezi kufa kwa utaratibu huo.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana mjini Chato mkoani Geita alipozungumza na viongozi wakuu wa vyombo hivyo vya ulinzi na usalama kuhusu hali ya ugonjwa wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19).

Aliwashukuru Watanzania kwa kuitikia wito wa kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo na kwa kushiriki katika siku tatu za kumwomba Mungu aliepushe taifa na janga hilo.

"Ninawapongeza madaktari na wauguzi walio mstari wa mbele katika kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wa corona.

"Ninatoa wito kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhakikisha inachukua tahadhari za kutosha kwa misaada ya vifaa vya uchunguzi wa Corona na vifaa vya kujikinga kuambukizwa au kuambukiza (barakoa) hasa baada ya baadhi yake kuhofiwa kusababisha maambukizo ya ugonjwa huo," aliagiza.

Rais pia alitoa wito kwa wenye viwanda nchini kuzalisha barakoa kwa ajili ya Watanzania na vifaa vingine vya kukabiliana na ugonjwa huo, yakiwamo mavazi ya watoa huduma na mashine za kupumulia kwa wagonjwa badala ya kutegemea vifaa hivyo kutoka nje ya nchi pekee.

Aliwataka viongozi kujihadhari na baadhi ya njia zinazotumika kukabiliana na ugonjwa huo, ikiwamo kupulizia mitaa na majengo kwa kutumia kemikali zisizokuwa na uwezo wa kuua virusi vya Corona kama ilivyofanyika kwa baadhi ya mikoa nchini, na badala yake wasisitize njia za uhakika za kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema hatua zilizochukuliwa hivi karibuni za kupuliza kemikali katika baadhi ya mitaa ya Jiji la Dar es Salaam kwa lengo la kuua virusi vya corona 'ni upuuzi mtupu' na akaagiza uchunguzi ufanyike dhidi ya wahusika.

Alisema vyombo vya dola vinapaswa kumchunguza aliyetoa uamuzi huo, akihoji sababu za jiji hilo kuwa na idadi kubwa ya watu walioambukizwa virusi licha ya kupulizwa kwa kemikali hizo huku akionyesha shaka kwa upuliziaji kutumika kueneza virusi hivyo.

Rais Magufuli pia alisema serikali haitawafungia wananchi majumbani (lockdown) wala kulifunga Jiji la Dar es Salaam ili kuepusha madhara makubwa yanayoweza kuwakumba wananchi na kuathiri uchumi wa nchi.

Aliwataka Watanzania kuondoa hofu, kuendelea kuchukua tahadhari huku wakiendelea na shughuli zao za uzalishaji mali na ujenzi wa taifa.

"Tuwaondoe hofu wananchi, siyo ugonjwa huu pekee unaosababisha vifo kwa wananchi, na siyo kila anayepoteza maisha hivi sasa basi amekufa kwa Corona.

"Nimejulishwa takwimu za mpaka jana (juzi) idadi ya walioambukizwa ni 284 na kati yao takribani 100 wamepona, tuwaambie wananchi kuhusu taarifa hizi badala ya kuwaacha wanajawa na hofu, hali inayoleta madhara zaidi," alionya.

Aliwataka viongozi wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wanaosababisha hofu kwa wananchi na kusambaza taarifa zisizo sahihi wakiwamo wanasiasa ambao aliwataka kuacha kutafuta umaarufu wa kisiasa kupitia janga hilo, na badala yake Watanzania wote waungane kupambana nalo.

Vilevile, Rais Magufuli alitoa wito kwa nchi zote za Afrika kuungana kuziomba taasisi za kifedha za kimataifa, ikiwamo Benki ya Dunia (WB), ambazo zimetangaza kusaidia mataifa ya Afrika, kutoa msamaha wa madeni badala ya kutaka kukopesha mikopo mingine ilhali nchi hizo zinakabiliwa na madeni ya mikopo ya zamani.

Kabla ya kikao hicho, Rais Magufuli alimwapisha Prof. Mabula Mchembe kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Rais alisema amefanya mabadiliko hayo ili kuongeza kasi ya utendaji katika wizara hiyo ikiwamo kukabiliana na virusi vya corona.

**TOLEO MAALUM**



## DK. REGINALD ABRAHAM MENGI

*"Bila wazo bora la kibiashara, hata kama ukipata Shilingi milioni 100 huwezi kufanikiwa kibiashara."*

# Subhash: Dk. Mengi alipigania uchumi wa viwanda nchini

**Na Romana Mallya**

SHIRIKISHO la Viwanda Tanzania (CTI), limeandika kitabu kumuenzi Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, kutambua mchango wake wa kuhakikisha nchi inafikia uchumi wa viwanda.

Mwenyekiti wa CTI, Subhash Patel, anamuelezea Dk. Mengi alivyoshiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo katika sekta ya viwanda.

Anasema alikuwa Mwenyekiti wa Shirikisho hilo na kati ya waanzilishi wa CTI ambayo lengo lake lilikuwa kusaidia, kujadili na kushirikiana na serikali mambo mbalimbali ya maendeleo ya viwanda kwa faida ya pande hizo mbili.

Kitabu hicho kinatarajiwa kuzinduliwa mwaka huu, chenye jina la 'Buy Tanzania, Build Tanzania' (Nunua Tanzania, Jenga Tanzania).

Akiwa miongoni mwa wafanyabiashara wakubwa nchini, Patel ambaye pia ni Mwenyekiti wa Motisun Group inayojihusisha na utengenezaji wa bidhaa tofati zikiwamo nondo, anasema katika kitabu hicho, CTI imempa kurasa mbili Dk. Mengi ili kutaja baadhi ya mambo aliyosaidia Shirikisho hilo, jamii na nchi kwa ujumla.

"Tutamuenzi kupitia kurasa hizo mbili na mafanikio aliyoyafanya kuiwezesha CTI kufika hapa ilipo, kitabu hiki tunatarajia kukizindua kabla ya uchaguzi mkuu mwaka huu, unaotarajia kufanyika mwezi Oktoba.

Kitabu hicho anasema kinawakumbusha Watanzania kupenda vinavyozalishwa nchini mwao ili waweze kuijenga nchi yao.

"Yapo mengi ndani yake ambayo wakati wa uzinduzi Watanzania wataweza kuyafahamu, ni kitabu kilichobeba uzalendo zaidi kwa Watanzania kujivunia vya kwao kabla ya vile vinavyotoka nje ya nchi, na Dk. Mengi alisisitiza hili mara kwa mara."

Angependa kabla ya tuzo ya Rais ambayo CTI huitoa kila mwaka, kukitoa kitabu hicho ambacho kitatangaza sifa ya viwanda vya Tanzania.

"Kwa sasa kipo kwa mchapishaji tunataka wakati wa tuzo ya Rais tuwe nacho. Serikali imetamka nchi ya viwanda ifikapo mwaka 2025, mchango wa CTI kwenye hilo ni mkubwa.

"Wenyeviti wa CTI waliopita ni wengi, lakini Dk. Mengi alikuwa mtu wa watu, aliwezesha watu wengi kujisaidia katika maisha yao, alikuwa na viwanda vyake mwenyewe, alipenda nchi ikifika mwaka 2025 iwe kwenye uchumi wa kati ili tulenge viwanda."

"Wenyekiti wengine watakaoongoza CTI katika hatua ya viwanda mpaka mwaka 2025, ninawaombea kwa Mungu wasimsahau Dk. Mengi kwenye mafanikio na mchango wake mkubwa aliotoa kwa nchi na Watanzania kwa ujumla."



Mwenyekiti wa Shirikisho la wafanyabiashara Wenye Viwanda nchini Subhash Patel akizungumza mara baada ya kuchaguliwa. **NA MPIGAPICHA WETU**

> "Vijana mjinyime starehe na mkiwekeza kwenye maendeleo mtafanikiwa, usitake kupata fedha kidogo unaanza kununua saa nzuri, shati zuri, nyumba nzuri, gari la kifahari.

**HAKUWA MBAGUZI**

Dk. Mengi kwake ni kaka, amejifunza mengi kwa sababu alikuwa anazungumza naye mara kwa mara.

"Nilikuwa nazungumza naye na kushirikishana hisia, ni mtu wa watu, akiona watu wasio na uwezo anakuwa chachu kubwa kuwasaidia, kama mwanadamu anakuwa mbele kuchangia katika dhoruba yoyote kwenye nchi."

"Alikuwa ni mfano wa uzalendo ambao mwanadamu anatakiwa kuwa, mimi ni Baniani yeye ni Mwafrika, lakini alikuwa hachagui rangi, dini wala kabila, alikuwa anataka maendeleo ya nchi."

"Nimesafiri na Dk. Mengi, kaka Juma Mapachu (Balozi), kwenda nchi mbalimbali duniani ikiwamo Zimbabwe, Ujerumani na Afrika Kusini, katika msafara wa serikali ama Waziri Mkuu au Rais, mchango wa Dk. Mengi aliweka nchi mbele siyo ubinafsi. Hii ndiyo imefanya awe mtu wa watu."

Patel anasema katika jambo lililohusu taifa, Dk. Mengi alilifanya kwa kuhakikisha maslahi yake binafsi anayaweka kando na ya nchi na wananchi aliyaweka mbele.

**WATANZANIA WAJIFUNZE**

Watanzania wanatakiwa kuchukua mfano wa Dk. Mengi, namna alivyoanza maisha yake baada ya elimu ndogo.

"Ukisoma kitabu chake cha 'I Can, I Must, I Will' kuna kitu kikubwa ndani yake kwa Mtanzania yeyote ambaye anataka kuwa na maendeleo, anajifunza kuwa uwezo anao, dhamira anayo na atafanya."

"Kweli kwenye maisha yake amefanya mengi kama jina lake, amefanya mengi na amekuza Tanzania kuwa katika sehemu nzuri kimataifa, Dk. Mengi siyo Mtanzania tu, aliweka utu na utanzania wake.

"Ninamfahamu tangu ameanza kujaza kalamu, wakati huo, nilikuwa ninaanza maisha yangu, akahamia Pugu Road kwenye ghala dogo akiwa na mfanyabiashara Bagwanji maarufu kama Bhaga ambaye alikuwa mfanyabiashara mshirika."

"Watanzania lazima wajue, Dk. Mengi hakuanza biashara akiwa tajiri mkubwa, alianza biashara ndogo amekuwa mpaka anakuwa na viwanda vyake na media yake.

"Hatukumtegemea mtu anaanza na kalamu mpaka anafika hapo alipofika. Wakati ninaanza viwanda vyangu vya chuma, plastiki alikuwa akinipa ari na moyo alikuwa akiniambia hayo ndiyo mahitaji ya nchi."

"Aliniambia nijitahidi nifanikiwe, huo moyo bila kukupa fedha unatosha kwa mwanadamu kumwezesha kuvuka mto salama, alinitia moyo nikavuka." Anasema.

**FUNZO KWA VIJANA**

Patel amewataka vijana wa Tanzania wanaotaka kufikia mafanikio na kuiwezesha nchi kufikia maendeleo ya viwanda lazima wakubali kujinyima starehe.

"Vijana mjinyime starehe na mkiwekeza kwenye maendeleo mtafanikiwa, usitake kupata fedha kidogo unaanza kununua saa nzuri, shati zuri, nyumba nzuri, gari la kifahari."

"Wekeza kwanza kwenye kitu cha kukuendeleza, fikra yako na muda wako uwe kwenye kitu cha kukuendeleza siyo kwenye vitu vya anasa, vijana wakijituma maendeleo yatakuwapo, nchi hii bado ina nafasi nyingi za kuwekeza.

"Nafasi za kujituma zipo nyingi, vijana mshindwe wenyewe, hata Dk. Mengi mnamuona ni miongoni mwa matajiri, yote ni kwa sababu, ujana wake alijitoka kuwekeza kwenye vitu vya maendeleo."

"Hakuwekeza kwenye kununua shati zuri, nyumba nzuri, gari la kifahari, haya yalikuja baadaye baada ya mafanikio yake binafsi na kwa nchi yake."

# Usajili mpya wa wanahabari waja

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA, MJINI

SERIKALI imewataka waandishi wa habari nchini kujiendeleza kitaaluma ili kukidhi vigezo vya Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016, inayowataka ifikapo 2021 kuwa na elimu ya stashahada (diploma).Akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema sheria ilitoa kipindi cha miaka mitano kwa kila mwanahabari kuwa na kiwango hicho cha elimu na kitafika kikomo mwakani.

"Kwa kuwa kipindi hiki cha miaka mitano kinakwisha mwezi Desemba 2021, natoa wito kwa waandishi wa habari ambao bado hawajajiendeleza kielimu, ili kukidhi matakwa ya sheria wafanye, hivyo ili kuendelea na kazi ya uandishi wa habari baada ya muda huu wa mpito kuisha," alisema.

Waziri Mwakyembe alisema Wizara ipo katika hatua za mwisho za uanzishwaji wa Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, ikiwamo Baraza Huru la Habari ambalo litaundwa na wanahabari wenyewe baada ya kuanzishwa kwa bodi hiyo.

"Majukumu ya Baraza hili ni pamoja na kuandaa Kanuni za Maadili ya Taaluma ya Wanahabari kwa kushirikiana na Bodi ya Ithibati na kushughulikia malalamiko mbalimbali ya maudhui chini ya Kamati ya Malalamiko iliyoundwa ndani ya baraza," alisema.

Alisema hadi kufikia Machi mwaka huu, magazeti na majarida 233 yalisajiliwa ili kupanua wigo wa upatikanaji wa habari kwa wananchi, na kwamba kati yake binafsi ni 181 sawa na asilimia 78 na serikali na taasisi zake 52, sawa na asilimia 22.

Alisema leseni mpya 18 zilitolewa kwa ajili ya magazeti/majarida ambapo 14 zilitolewa kwa wamiliki binafsi na nne kwa taasisi za umma, na kwamba leseni 43 zilihuishwa, ikiwamo kutoa vitambulisho kwa wanahabari 494.

Kati yao, saba ni wa nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Peter Serukamba, alisema kuwa hadi kufikia Februari mwaka huu, wizara ilikuwa haijafikia hata nusu ya lengo la makusanyo kwa kuwa ilikuwa imekusanya Sh. bilioni 14.5, sawa na asilimia 37.7 ya lengo.

Naibu Waziri Kivuli katika wizara hiyo na Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Devotha Minja, alitaka Wizara ya Afya kutoa taarifa za corona kila baada ya saa kadhaa ili kuendeleza tahadhari.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.
(Together, we can build a better life)

UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2020 (*Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2020 | Robo Mwaka iliopita 31 Desemba 2019 |
|---|---|---|---|---|
| A | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 796.63 | 405.33 |
| | 2 | Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 17,653.40 | 6,601.31 |
| | 3 | Uwekezaji katika Amana za serikali | 18,619.79 | 25,371.80 |
| | 4 | Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 777.39 | 668.44 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 61.95 | 67.32 |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| | 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 30,836.28 | 36,866.46 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 38,521.20 | 35,634.01 |
| | 12 | Mali Nyingine | 857.05 | 838.23 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| | 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,452.86 | 1,556.18 |
| | 16 | **JUMLA YA MALI** | **109,576.53** | **108,009.07** |
| B | | **DHIMA** | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 29,050.00 | 32,500.00 |
| | 18 | Amana za Wateja | 42,081.30 | 37,399.46 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | 20 | Amana Maalumu | - | - |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,137.08 | 1,302.99 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa | - | - |
| | 27 | Dhima Nyingine | 819.25 | 839.34 |
| | 28 | Madeni | - | - |
| | 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **73,087.63** | **72,041.79** |
| | 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29*** | **36,488.90** | **35,967.28** |
| C | | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | 788.02 | 828.58 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 2,349.26 | 836.39 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 521.62 | 1,472.31 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| | 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **36,488.90** | **35,967.28** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 14,538.72 | 10,781.42 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 4,032.28 | 4,125.84 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 282.27 | 162.90 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 33.30% | 33.30% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 10.42% | 11.49% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 54.41% | 51.14% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 35.51% | 33.24% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81.00% | 91.23% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | 1.76% | 5.01% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | 1.45% | 5.60% |

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 14-04-2020 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 14-04-2020 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 14-04-2020 |

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 MACHI 2020

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2020 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 31 Machi 2019 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Machi 2020 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31Machi 2019 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 2,128.43 | 1,836.15 | 2,128.43 | 1,836.15 |
| 2 | Gharama za Riba | 781.62 | 541.05 | 781.62 | 541.05 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,346.81** | **1,295.10** | **1,346.81** | **1,295.10** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 119.37 | 60.00 | 119.37 | 60.00 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **192.02** | **195.09** | **192.02** | **195.09** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 35.93 | 51.18 | 35.93 | 51.18 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 156.09 | 143.91 | 156.09 | 143.91 |
| | 6.3 Gawio | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **687.84** | **1,058.75** | **687.84** | **1,058.75** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 320.14 | 337.26 | 320.14 | 337.26 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 367.69 | 721.49 | 367.69 | 721.49 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **731.62** | **371.44** | **731.62** | **371.44** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 210.00 | 120.00 | 210.00 | 120.00 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **521.62** | **251.44** | **521.62** | **251.44** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 25 | 20 | 25 | 20 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 16 | 8 | 16 | 8 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 16 | 8 | 16 | 8 |
| 14 | **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.48% | 0.25% | 0.48% | 0.25% |
| (II) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.44% | 0.73% | 1.44% | 0.73% |
| (III) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 29.64% | 52.12% | 29.64% | 52.12% |
| (IV) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.75% | 5.64% | 5.75% | 5.64% |

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 14-04-2020 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 14-04-2020 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 14-04-2020 |

TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 MACHI 2020 *(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2020 | Robo Mwaka iliopita 31 Desemba 2019 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Machi 2020 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31Machi 2019 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 521.62 | 1,472.31 | 521.62 | 251.43 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| | Hasara katika mali | 111.70 | 1,300.77 | 111.70 | 240.00 |
| | -Badiliko halisi katika Mikopo | (2,887.18) | (842.93) | (2,887.18) | 3,052.34 |
| | Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika Amana | 1,231.84 | 3,336.53 | 1,231.84 | (4,984.43) |
| | Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 98.60 | 794.93 | 98.60 | (242.34) |
| | Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 77.05 | (931.66) | 77.05 | 181.23 |
| | Kodi iliyolipwa | (210.00) | (612.79) | (210.00) | - |
| | Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(1,056.37)** | **4,517.15** | **(1,056.37)** | **(1,501.77)** |
| II | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za kudumu | (8.38) | (19.39) | (8.38) | (6.75) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | 6,751.93 | 978.16 | 6,751.93 | (3,564.55) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **6,743.55** | **958.77** | **6,743.55** | **(3,571.30)** |
| III | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo(bainisha) | (74.57) | (346.31) | (74.57) | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(74.57)** | **(346.31)** | **(74.57)** | **-** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 5,612.61 | 5,129.61 | 5,612.61 | (5,073.07) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 48,369.87 | 43,240.26 | 48,369.87 | 42,092.56 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **53,982.48** | **48,369.87** | **53,982.48** | **37,019.49** |

TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI
KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 Machi 202031 DESEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo Mwaka wa sasa 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa Robo mwaka** | **32,830.00** | **-** | **2,308.69** | **828.58** | **-** | **-** | **35,967.28** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 521.62 | - | - | - | **521.62** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 40.56 | (40.56) | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | **-** | **2,870.88** | **788.02** | **-** | **-** | **36,488.90** |
| **Mwaka Uliopita 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **1,125.67** | **45.93** | **493.37** | **-** | **34,494.97** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,472.31 | - | - | - | **1,472.31** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (782.65) | 782.65 | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 493.37 | - | (493.37) | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | **-** | **2,308.69** | **828.58** | **-** | **-** | **35,967.28** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2020**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 14-04-2020 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 14-04-2020 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 14-04-2020 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| 1. SANTANU KUMAR MAJUMDAR | MJUMBE WA BODI | (Imesainiwa) (Imesainiwa) | 14-04-2020 |
| 2. RAJAB SELEMAN KAKUSA | MJUMBE WA BODI | | 14-04-2020 |

Canara Bank (T) Ltd
Head Office Dar Es Salaam Branch
Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania
E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532
www.canarabank.co.tz


## Masharti yalegezwa ununuzi wa madini

**Na Augusta Njoj,** DODOMA

SERIKALI imelegeza masharti ya ununuaji madini kutokana na janga la ugonjwa wa corona, huku ikiruhusu mtu yeyote mwenye mtaji wa kununua afuate taratibu zilizowekwa.

Sambamba na hilo, imefanya mazungumzo na mabenki kwa lengo la kuwapatia fedha wanunuzi wa madini ili kununua madini.

Akihitimisha hoja ya bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka 2020/21 bungeni juzi, Waziri Doto Biteko, alikiri kuwa licha ya bei ya madini ya dhahabu duniani kupanda, lakini wafanyabiashara wa ndani hawana fedha za kununua madini yaliyopo kwa wachimbaji.

"Wafanyabiashara hawa fedha zimekwisha, maana wanachokifanya ni kwamba, wanunuzi wa ndani hununua na kwenda kuuza nje, wanapata fedha wananunua tena, lakini kutokana na huu ugonjwa, kwa sasa hawasafirishi hivyo wamenunua, wana mzigo, lakini fedha za kununua tena hawana," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo Wizara imeangalia namna ya kulegeza ili mzunguko uwapo. "Hivyo mfanyabiashara yeyote mwenye fedha aje, aende kununua mahali popote, naomba nitoe tangazo hili, ule utaratibu wa kununua kwa kanda tunaouvuka, mfanyabiashara yeyote aende mahali popote kwenye soko lolote anunue dhahabu atapewa vibali vyote vinavyohitajika bila kujali mpaka wake,"alisisitiza.

Kuhusu mazungumzo na mabenki, alisema wamezungumza na mabenki na yamekubali kukaa na wanunuzi wa madini ili kuwapatia fedha.

"Pia masharti tumelegeza mtu yeyote sasa mwenye mtaji aende kununua madini ilimradi analipa mrabaha na pale atakapotunza serikali itajua ametunza wapi na ya thamani gani," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Majaliwa aagiza msako wanaouza sukari bei juu

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaagiza wakuu wa mikoa kuchukulia hatua dhidi ya wafanyabiashara waliopandisha bei ya sukari na kufikia Sh. 4,500 kwa kilo.

Amesema haoni sababu ya kupanda kwa bei kwa kuwa bidhaa hiyo ipo ya kutosha nchini.

Hatua hiyo inakuja ikiwa ni wiki sasa tangu sukari kupandishwa bei maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza na viongozi wa dini waliojitokeza kwenye maombi maalum kwa kitaifa dhidi ya virusi vya corona jijini Dar es Salaam jana, Majaliwa aliwataka wafanyabiashara kutopandisha bei ya sukari na bidhaa nyingine.

"Sukari ipo, tena ya kutosha na iliyokuwa imepungua imeshaagizwa na imeingia nchini, bei inaendelea kuwa ileile, viwanda vya ndani vikianza kuzalisha, bei itaendelea kuwa ileile," Majaliwa alisema.

Alisema ameona kwenye mitandao kilo imefikia Sh.4,500 na kuwaagiza wakuu wa mikoa kuwachukulia hatua wafanyabiashara hao.

"Nitoe wito kwa wafanyabiashara kama nilivyoesma, wiki hii Waislamu wanatarajia kuanza mfungo wa Ramadhani, wafanyabiashara kote nchini wahakikishe uhitaji wa vyakula muhimu kwenye kipindi hiki cha Ramadhani vinauzwa kwa bei inayotambulika bila kupandishwa.

"Kwa kufanya hivyo, tunawakwaza Watanzania, tunawakwaza Waislamu, ninatoa maelekezo kwa wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kufanya ziara za mara kwa mara kwenye masoko yetu.

"Hakuna sababu ya kupandisha huduma kwenye masoko eti kwa sababu baadhi ya Watanzania wanaingia mwezi Mtukufu."

Waziri Mkuu pia aliwataka Waislamu wanaotarajia kuanza mfungo wa Ramadhan kujiepusha na misongamano kipindi hiki ambacho kuna mlipuko wa corona.

Wiki iliyopita, Nipashe ilibaini gharama za kuagiza bidhaa hiyo nje ya nchi zinafikia Dola 757.47 (Sh. 1,748,080) kwa tani moja.

Mchanganuo wake ni: Cost+insurance+freight Dola 425 (Sh. 980,810) kwa tani, duty (35%) Dola 148.75 (Sh. 343,283) kwa tani, VAT (18%) Dola 104.82 (Sh. 241,902), clearing and transport Dola 70.29 (Sh.162,214) kwa tani.

"Kwa mantiki hiyo, mfuko wa Kg 50 wa sukari unagharimu Dola 37.8 (Sh. 87,677) na ukijumulisha na faida ya asilimia nane (7,400), unaona kwamba mfuko huo unapaswa kuuzwa kwa Sh. 95,000 (Sh. 1,900 kwa kilo) na si 130,000 inayofanyika sasa," alisema mmoja wa wafanyabiashara wa sukari ambaye aliomba hifadhi ya jina lake.

## JPM ateua watendaji wapya

**Na Mwandishi Maalum, CHATO**

RAIS John Magufuli, amemteua Dk. Zainab Chaula, kuwa Katibu Mkuu wa Mawasiliano.

Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu ilisema jana kuwa kabla ya uteuzi huo, Dk. Chaula alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na amechukua nafasi iliyoachwa na Dk. Maria Sasabo, ambaye amestaafu.

Rais Magufuli pia amemteua Prof. Mabula Mchembe kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Kabla ya uteuzi huo, Prof. Mchembe alikuwa Msaidizi wa Rais katika masuala ya afya.

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli amemteua Prof. Abel Makubi, kuwa Mganga Mkuu wa Serikali (Chief Medical Officer).

Kabla ya uteuzi huo, Prof. Abel Makubi, alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando na amechukua nafasi iliyoachwa, na Prof. Mohamed Kambi ambaye amestaafu.

Katika taarifa hiyo ya Ikulu, ilielezwa kuwa uteuzi wa viongozi hao ulianza jana.


**Canara Bank (Tanzania) Ltd.**
(Together we can build a better life)

**DISCLOSURE UNDER REGULATION 12 OF BANKING & FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS 2014**

**CUSTOMER COMPLAINT REDRESSAL MECHANISM: To The Esteemed Customers Canara Bank (Tanzania) Ltd Tanzania**

**1. INTRODUCTION (UTANGULIZI)**

The Complaints Resolution Desk (the Desk) has been established by the Bank of Tanzania (BOT) as a cost effective and efficient mechanism to resolve complaints between banking institutions and their customers. The Desk, which is fully funded by the Bank, is intended to resolve complaints (small claims) whose monetary value in respect of both the claim amount and remedy awarded does not exceed fifteen million Tanzania shillings (15,000,000) Mn.

**2. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH OUR BANK (JINSI YA KUWASILISHA MALALAMIKO KWA DAWATI)**

When you are dissatisfied with our services or you have any complaint pertaining to our staff or bank or otherwise, you may lodge complaint to us in writing by post or fax or through your registered email address on the following contact addresses.

**General Manager (Operations) Canara Bank (Tanzania) Ltd,**
**Dar es Salaam Branch,**
**Post Box 491 Dar es Salaam**
**Phone : +255 (22) 2112532**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail : cbtl@canarabank.co.tz**

**The Nodal Officer, Grievance Redressal Cell,**
**Canara Bank (Tanzania) Ltd**
**Post Box 491 Dar es Salaam,**
**Phone : +255 (22) 2112530;**
**Fax: +255 (22)2112534**
**E Mail compliance.cbtl@canarabank.co.tz**

**NOTE:**
- For lodging complaint with BOT please use Complaint Form No 1.
- For detailed information for lodging compliant with BOT please visit BOT website https://www.bot-tz.org.

**3. INTERNAL COMPLIANT RESLUTION MECHANISM (MCHAKATO WA KUTAFUTA UFUMBUZI WA MALALAMIKO)**

We through our internal complaint handling mechanism shall resolve your complaints within 21 working days from the date of lodging the compliant. The Internal Complaint handling mechanism in our Bank is as under:
- Receiving and timely processing consumers' complaints.
- Keeping complainants updated throughout the process.
- Keeping a record of all complaints and submit it to the Bank of Tanzania on quarterly basis.
- Resolving all consumer complaints within 21 working days from the date of lodging the complaint.
- In exceptional circumstances if we are unable to resolve the complaint within 21 working days, we will immediately inform the complainant of our inability and reason for the inability and what measures are being taken to resolve the matter urgently and in any case not more than 14 working days thereafter.

**4. HOW TO LODGE A COMPLAINT WITH THE DESK AT BANK OF TANZANIA (BOT) (NAMNA YA KUWASILISHA LALAMIKO KWA DAWATI LA BOT)**

If you are dissatisfied with the decision of our Bank in respect of your compliant or do not receive a response from our Bank within 21 working days from the date of lodging your complaint, you may within 14 working days lodge your complaint with the Desk at BOT. However, before lodging your complaint with the Desk at BOT, you are required to exhaust the Internal Complaints resolution mechanism of our Bank first.

The compliant with Complaints Resolution Desk at Bank of Tanzania shall be lodged in the prescribed form (Schedule A), duly signed by the complainant and shall be submitted in any of the following ways:
a) By hand or by post to:
Complaint Resolution Desk
Office of the Secretary to the Bank of Tanzania,
10 Mirambo Street,
11884, Dar es Salaam.
b) By electronic mail: complaints-desk@bot.go.tz
d) By facsimile to fax no: +255 22 2234067
e) By phone: +255 22 2233265/ +255 22 2233246

**Note:**
a) Complaints shall be lodged with the Desk from 9.00 AM to 12.30 Pm (Monday to Friday).
b) Your complaint must be lodged before expiry of two years after the cause of action arose.

**5. PECUNIARY JURISDICTION OF THE BOT DESK (MAMLAKA ZA KIFEDHA ZA DAWATI)**

The desk shall handle complaints whose total monetary value in respect of both the claim amount and remedy to be awarded does not exceed Fifteen Million Tanzania Shillings (TZS 15,000,000/-).

**6. ELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YA HAKI)**

Only the following categories of complaints are eligible for submission to the Desk;
a) A complaint against a banking institution which is either a member of the Tanzania Bankers Association or regulated by the Bank.
b) A complaint which is lodged within 14 days after a banking institution has delivered its decision or has failed to respond.
c) A complaint in respect of an incident which occurred less than two (2) years ago.

**7. INELIGIBLE COMPLAINTS (MALALAMIKO YASIYO NA HAKI)**

In terms of the Guidelines issued, the Desk considers the following complaints as ineligible:
a) A complaint which has been the subject of legal proceedings before a Court or Tribunal.
b) Where the complainant has not suffered any financial loss, material inconvenience or distress.
c) A complaint which would be more suitably dealt with by a Court or under other dispute resolution arrangement.
d) A complaint whose resolution would prejudice the rights of other parties who have not consented to the resolution by the Desk.
e) A complaint which is vexatious or frivolous or not in good faith.
f) A complaint which was not first reported to the banking institution concerned.
g) A complaint which is lodged more than 14 days after a banking institution has delivered its decision or failed to resolve the complaint.
h) A complaint which is beyond the pecuniary jurisdiction of the Desk.

**8. INFORMATION YOU MUST INCLUDE IN THE COMPLAINT (TAARIFA MUHIMU ZA KUJUMUISHA KWENYE LALAMIKO)**
a) Your name and address.
b) The name and address of the banking institution against which the complaint is made.
c) Details of what your complaint is about including exactly what the bank did that it shouldn't have done or what it didn't do that it should have done.
d) What you have lost in terms of personal injustice, financial loss, hardship or inconvenience.
e) What you would like the Desk to do to put things right and details of what you have done so far to try to resolve the complaint
f) Include documentary evidence, if any.

**9. WITHDRAWAL OF THE COMPLAINT (KUFUTA LALAMIKO)**

A complainant may, at any time before the Desk's determination, withdraw his complaint in writing from the Desk, and the matter shall be closed by the Desk.

**10. FREE SERVICE (HUDUMA ZA BURE)**

Resolution of banking consumers' complaints is free of charge as the Desk does not charge any fee whatsoever.

**11. MEDIUM OF COMMUNICATION (NJIA YA MAWASILIANO)**

The medium of communication is both English and Kiswahili.

**12. REMEDIES AWARDED (SULUHISHO LILILOPATIKANA)**

The function performed by the Desk is different from that performed by courts. The Desk is enjoined not to have regard to technicality and legal form but resolve complaints using criteria that would not usually be used by courts; for instance whether an explanation for the conduct was not given when it should have been given. A banking institution may be required to issue an apology, change its practices, effect payment or compensation as the case may be. The Desk is not bound by the legal principles of handling complaints such as rules of evidence but adheres to the general principles of natural justice.

When Aggrieved by Desk decision

Either party may request the Desk to reconsider any of its decision. Each party also has a right to seek redress before a competent court when it is not satisfied with the decision given by the Desk

**CANARA BANK (TANZANIA) LIMITED**
**VIWANGO VYA TOZO NA HUDUMA KUANZIA 01/07/ 2018**

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| **A. AKAUNTI ZA AKIBA** | | |
| 1. Kufungua akaunti | 50,000 | 50 |
| 2. Ada ya huduma kila mwezi | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| 3. Akaunti kutokua na kima cha chini | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| 4. Tozo za taarifa ya akaunti | | |
| a) Mwezi | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| b) Kipindi fulani | 5,000.00 | $5 |
| 5. Tozo ya kutoa pesa kwenye akaunti | Hakuna tozo | Mpaka 5000 Hakuna tozo Above 5000 - 0.3% |
| 6. Tozo ya kuweka pesa kwenye akaunti | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| 7. Cheti cha kuhakiki salio | 15,000.00 | $7 |
| 8. Tozo ya kufunga akaunti | 15,000.00 | $15 |
| 9. Kufufua akaunti | 6,000.00 | $6 |
| **B. AKAUNTI ZA HUNDI** | | |
| 1. Kufungua akaunti | 100,000 | 100 |
| 2. Ada ya huduma kila mwezi | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| 3. Akaunti kutokua na kima cha chini | Hakuna tozo | Hakuna tozo |
| 4. Tozo za taarifa za akaunti a) Mwezi b) Mpito | 5000 5000+500 Kwa kila kurasa | $5 $ 5+1 kwa kila kurasa |
| 5. Tozo ya kutoa pesa kwenye akaunti | MPAKA 25 MIO-Hakuna tozo MPAKA 25 MIO--0.12% | Mpaka 5000 Hakuna tozo 5000 to 10,000 - 0.3% Zaidi 10,000 - 0.5% |
| 6. Tozo ya kuweka pesa kwenye akaunti | Zaidi 50 MIO- Hakuna tozo Zaidi 50 MIO-- 0.12% | Zaidi 10,000- Hakuna tozo > 10,000- 0.3% |
| 7. Cheti cha kuhakiki salio | 25,000.00 | $15 |
| 8. Agizo la kusimamisha malipo | 30,000.00 | $15 |
| 9. Hundi iliyokataliwa | | |
| a) Hundi ya ndani | 30,000.00 | $15 |
| b) Hundi ya nje | 30,000.00 | $20 |
| 10. Tozo kufunga Akaunti | 25,000.00 | $20 |
| **C. TOZO ZA MIAMALA YA SIMU** | | |
| 1. Kutoa pesa | | |
| Mpaka 100,000 | 2,000.00 | NA |
| 101,000 to 200,000 | 3,000.00 | NA |
| 201,000 to 400,000 | 5,000.00 | NA |
| 401,000 to 600,000 | 6,000.00 | NA |
| 601,000 to 999,000 | 8,000.00 | NA |
| 2. Kuhamisha fedha/Kuhamisha kwa njia ya mtandao wa simu | | |
| Mpaka 100,000 | 500.00 | NA |
| 101,000 to 250,000 | 1,000.00 | NA |
| 251,000 to 500,000 | 2,000.00 | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | 5,000.00 | NA |
| 1,001,000 MPAKA 10,000,000 | 10,000.00 | NA |
| **HUDUMA ZA KIBENKI** | | |
| A) Tozo za mwezi | 500.00 | NA |
| B) Kuomba namba ya siri | 2,500.00 | NA |
| **H. TOZO YA LOCKERS KWA MWAKA** | | |
| 1.NDOGO | 350,000.00 | |
| 2. SAIZI YA KATI | 600,000.00 | |
| 3. KUBWA | 750,000.00 | |

| D. KUHAMISHA FEDHA BAINA YA BENKI | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. TISS | 11,800.00 | $11.8 |
| 2. E Remittances | | |
| Mpaka USD 1,000 au Eq. TZS | 20,000.00 | $10 |
| 1001 mpaka 5000 | 24,000.00 | $12 |
| 5001 mpaka 10000 | 48,000.00 | $25 |
| 10,001 na zaidi | 100,000.00 | $50 |
| 3. SWIFT | | |
| a) Swift Outward | | |
| Mpaka 5,000 | NA | $45 |
| 5,001 mpaka 10,000 | NA | $60 |
| Zaidi 10,000 | NA | $90 |
| b) Swift Inward | | |
| Mpaka 5,000 | NA | $12 |
| 5,001 mpaka 10,000 | NA | $18 |
| Zaidi ya 10,000 | NA | $30 |
| **E. TOZO ZA MIKOPO** | | |
| 1. Ada ya kushughulikia mkopo | Mpaka 5 Mio - 25,000 5Mio mpaka 10 Mio - 200,000 10 Mio mpaka 25mio - 400,000 25 mio mpaka 500 mio - 1.5% >500mio-- 1.25%* *minimum 7.5mio | Mpaka 5,000 - $100 5000 to 10,000 - $200 Mpaka 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.5% >500,000--1.25%* *Kima cha chini 7,500 |
| 2. Nyaraka za mkopo | Mpaka 100 mio --NIL-- >100 Mio 0.3% -Min 300,000 | Mpaka 50,000 --NIL-- >50,000 - 0.3% Min 150 |
| 3. Mkopo wa muda-Malipo ya awali | Mpaka 5Mio - 25,000 5 Mio mpaka 10 Mio - 200,000 10Mio 25mio - 450,000 25 mn to 500 mio -1.8% >500mio--1.5%* *minimum 9mio | Mpaka 20,000 - $300 20,000 to 500,000 - 1.8% >500,000--1.5%* *kiwango cha chini 9000 |
| 4. Tozo ya ukaguzi | Mpaka 100 Mio -25,000 >100 mio - 50,000 | Mpaka 50,000 - 25 >50,000 ----50 |
| **F. LETTER OF CREDIT** | | |
| Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof) | | |
| Opening commission | NA | 1.2% ( Kiwango cha chini $ 200) |
| LC amendment Commission | NA | 0.4% ( Kiwango cha chini $50 Kiwango cha juu 350) |
| Swift charge for LC opening | NA | $40 |
| Swift charge for other message/amendments | NA | $40 |
| Extensions - Commissions | NA | .2% ( Kiwango cha chini $200) |
| LC cancellation charges | NA | .2% ( Kiwango cha chini $200) |
| Non payment of Bills on due date | NA | 16% Till Payment |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | |
| Advising commission | NA | $140 |
| Confirmation Commission | NA | 0.5% ( Kiwango cha chini $150) |
| Negotiating bills under LC | NA | 0.5%(Kiwango cha chini $75+cuourier+int) |
| Reimbursement claim paid | NA | 0.5% ( Kiwango cha chini $75) |
| Extensions - Commissions | NA | 1.2% ( Kiwango cha chini $200) |
| Collection of Export LC | NA | 0.5%(Kiwango cha chini $75+cuourier+int) |
| Amendments | NA | $75 |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | |
| Bonds & Guarantees | 1.2% ( Kima cha chini TZS 75,000) | 1.20% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | 0.5% kwa robo mwaka (Min TZS 75,000) | 40% gharama halisi |

CANARA BANK (TANZANIA) LIMITED
16/1, ELIA COMPLEX , ZANAKI BIBI TITI STREET
POST BOX NO 491, DAR ES SALAAM, TANZANIA
TEL : 255 22 2112530/31/32/34

**Banking Services offered BY Canara Bank (Tanzania) Ltd** **We offer following Services**

- Current and Saving Account
- Salary Account
- Student Account
- Fixed Deposit Account
- Re Investment Deposit Account
- Recurring Deposit Account
- Overdraft and Term Loans
- Vehicle Loan
- Mortgage Loan
- Personal Loan
- Insurance Premium Funding
- Safe Deposit Lockers
- All Export and Import Related transactions
- Letter of Credit and Guarantees
- E- Remit Facility to India
- Mobile Banking




Plot No 16/1, Elia Complex
Zanaki-Bibi Titi Street, P.O.Box 491- Dar es Salaam, Tanzania
T: +255 222 112 2530 (D) +255 222 112 532
Email: cbtl@canarabank.co.tz

**Access your A/c 24x7**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ahadi hii kwa wastaafu itelekezwe kwa vitendo

**WASTAAFU** wengi hususan wa umma wamekuwa wakikumbana na kikwazo cha kulipwa mafao yao baada ya kustaafu utumishi.

Hali hiyo imesababisha baadhi kufariki dunia kabla ya kupata mafao yao bila sababu ya kutokulipwa stahiki zao kwa wakati kuwekwa wazi.

Mpaka sasa kuna idadi kubwa ya wastaafu wa sekta ya umma wako mitaani wakihangaikia kufuatilia malipo yao, huku wakilazimika kutumia gharama zaidi kuliko uwezo wao kifedha.

Maelekezo ambayo wamekuwa wakipewa na maofisa utumishi ni kuwa sasa waende kufuatilia Dodoma kutokana na serikali kuhamia humo.

Kimsingi, wastaafu wanateseka sana kufuatilia haki zao, kiasi kwamba inafika wakati wanakata tamaa na kujiona kuwa utumishi wao ulioendana na weledi, uzalendo, uaminifu na uadilifu hauthaminiwi na serikali.

Hata hivyo, maelekezo yaliyotolewa juzi na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yamedhihirisha kuwa serikali haifurahishwi kuona wastaafu wakitesekea mafao yao.

Waziri wa Ofisi hiyo, George Mkuchuka, amesema amepanga kukutana na maofisa utumishi wote nchini kuwakumbusha na kuwasisitiza umuhimu wa kuandaa mapema taarifa za mtumishi anayetarajia kustaafu miezi sita kabla ya kustaafu.

Mkuchuka anasema kwamba lengo la hatua hiyo ni kuondoa tatizo la ucheleweshwaji wa mafao, ambapo baadhi yao hufariki bila kuyapata.

Mkuchika, ndiye alisema hayo alipokuwa akitoa ufafanuzi wa namna atakavyotekeleza ahadi aliyoitoa bungeni ya kuhakikisha ofisi yake inatatua changamoto ya ucheleweshwaji wa mafao ya wastaafu wakati akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Waziri Mkuchika alisema anakwazwa na kitendo cha wastaafu walioitumikia nchi kwa uadilifu na uzalendo kuchelewa kupata mafao yao kwa wakati.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, wastaafu wamekuwa wakicheleweshewa mafao yao kuanzia mwaka mmoja hadi minne na wengine kufariki bila kuyapata.Alisema katika kipindi cha uongozi wake amebaini kuwa tatizo la wastaafu kuchelewa kupata mafao linasababishwa na baadhi ya maofisa utumishi kuchelewa kuandaa taarifa za wastaafu mapema na kuziwasilisha kwenye mamlaka husika, ikiwamo kitendo cha baadhi ya waajiri kutowasilisha michango ya watumishi kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii.


Kadhalika, Mkuchika aliwapiga marufuku maofisa hao kuwaelekeza wastaafu kufuatilia mafao yao jijini Dodoma au Dar es Salaam, badala yake wao ndio wabebe jukumu hilo kwa kuwa wastaafu wengi wanapata usumbufu na kukabiliwa changamoto ya ukosefu wa fedha.

Aliwataka maofisa hao kuwajibika ipasavyo na ikitokea mstaafu amechelewa kupata mafao yake, Ofisa Utumishi ndiye atatakiwa kuieleza serikali sababu za mstaafu huyo kutopata mafao yake kwa wakati, ikizingatiwa kuwa serikali imeshawaelekeza maofisa hao kuandaa taarifa za watumishi wanaotarajiwa kustaafu mapema iwezekanavyo. Alisema ofisi yake inahusika na utawala bora, hivyo itahakikisha mstaafu analipwa stahili zake kwa wakati na kitendo cha mstaafu kukaa miaka minne bila kulipwa mafao hakiakisi dhana halisi ya utawala bora.

Kwa mujibu wa maelezo ya Waziri Mkuchika, wanaochangia wastaafu kutokulipwa mafao yao kwa wakati mwafaka ni maofisa utumishi, hivyo kwa kuwa Waziri hiyo anakijua hilo, tunaamini kwamba sasa mwarobaini wa kutocheleweshwa malipo hayo umepatikana.

Hatuoni sababu za serikali kutowachukulia hatua kali za kisheria na kimaadili maofisa utumishi watakaobainika kuchelewa kuandaa malipo ya wastaafu kwa muda walioelekezwa, hivyo kuwasababishia usumbufu, taabu na mateso wastaafu hao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tuamke, tusisubiri kusukumwa kujikinga na vita vya corona

Na Sabato Kasika

**VIRUSI** vya corona ni janga ambalo limezikumba nchi nyingi duniani, Watanzania tukiwamo. Pia, juhudi zinandelea kuchukuliwa kukabiliana na na virusi hivyo, ambavyo bado havina dawa wala tiba.

Mkoa wa Dar es Salaam unatajwa kuwa kinara wa maambukizi ya virusi hivyo, na hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa na viongozi wa serikali, kukabiliana na janga hilo.

Katika hilo, Mkuu wa Mkoa, Paul Makonda, anawataka wakazi wa jiji kuvaa barakoa kuanzia wanapokuwa katika usafiri wa daladala, pia kwenye shughuli nyingine za kila siku au majumbani.

Katika jitihada hizo, ameagiza hata mfumo wa kufanya biashara ubadilike, ili kwamba mtu anapokwenda sehemu kununua vitu achukue na kuondoka na siyo anakaa muda mrefu usio na lazima.

Hizo zote ni juhudi za kutaka kukabiliana na corona. Msisitizo wa Mkuu wa Mkoa unajikita katika kuhakikisha kila mkazi wa jijini Dar es Salaam anavaa barakoa, huku akiepuka msongamano usio wa lazima.

Ni bahati nzuri, kile ambacho mkuu huyo wa mkoa amekiagiza, kimeanza kutekelezwa hasa kwa watu kuvaa barakoa, sambamba na wito wa awali wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuagiza watu wanawe mikono kwa maji yanayotiririka na kutumia vitakasa mikono.

Kinachoonekana awali, wengi wameitikia kilichoagizwa na serikali katika ngazi tofauti.

Ni ukweli kwamba tangu Jumatatu wiki hii, takrban kila mahali watu walianza kuvaa barakoa, hata wengine kujifunika vitambaa usoni kama njia ya kujikinga maambukizi ya virusi hivyo.

Kuanzia Jumatatu, ndiyo ambayo Makonda alikuwa ametangaza kuwa "yoyote ambaye angeonekana hajavaa barakoa, basi akamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria."

Inaonekana maelekezo hayo yameuingia umma na wanavaa vifaa hivyo haraka. ingawa kila mmoja alipaswa kutambua madhara ya corona na kuchukua hatua mapema badala ya kusubiri kutishiwa.

Kwa utekelezaji huo, ni wazi bado kuna watu hawana woga kuhusu janga hili linaloendelea kuitesa dunia hadi watishiwe ndipo wachukue hatua! Nasema, huku ni kupuuzia mambo ya hatari.

Umefika wakati sasa, kila mmoja wetu abadilike na kuacha kufanya mzaha kwenye mambo mazito kama hayo ya ugonjwa wa corona, ambao hivi sasa sote tunajua hatari yake kwa maisha.

Wataalam wa afya wanaeleza, anaweza kuvaa barakoa za vitambaa vya pamba, lakini zikiwa zimeongezewa uzito katika utengenezaji, ili kuruhusu kufanyiwa usafi wa kila mara inafuliwa kwa maji na sabuni na kisha inapigwa pasi.

Kwa maana hiyo, barakoa zinaweza kupatikana kwa gharama nafuu, hivyo sidhani hoja ya kukosa fedha za kununua, inaweza kuwa na mashiko kwa wengi.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, anasema, ingawa barakoa hizo hazina ubora wa kinga kama N-95 au zile za chumba cha upasuaji, lakini zinaweza kutumika kupunguza uwezekano wa maambukizi toka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

Kwa maana hiyo, watu wasiishie kufunika nyuso kwa vitambaa vya kupangusia jasho, badala yake wajishonee barakoa hizo ili angalau wajikinge na kuwakinga wengine.

Kuogopa kukamatwa kwa kutovaa barakoa ni sawa na kutoogopa ugonjwa huo, ambao umekuwa tishio katika nchi mbalimbali duniani. Hivyo haina haja kusukumwa bali tahadhari ni ya muhimu.

Suala la kujiongeza ni la msingi, hasa wakati huu wa hatari kuliko kusubiri kutishwa, ndipo mtu achukue hatua, kwani inaonekana ni kama anafanya kwa kushinikizwa na virusi badala ya kushinikizwa na ugonjwa.

Maelekezo yametolewa kwa muda mrefu ya jinsi ya kujikinga, lakini hadi Jumatatu wiki hii, ndipo watu wengi wamechukua hatua baada ya kutishiwa kukamatwa kana kwamba, kukamatwa ni hatari kuliko corona!

Vilevile bado kuna tatizo lingine ambalo ni muhimu watu walizingatie, kunawa mikono na kuzingatia umbali kati ya mtu mmoja na mwingine, kuepuka kuambukizana.

Ni bahati mbaya baadhi ya watu na hasa wachuuzi wadogo kando ya barabara, wako katika namna kama hawana habari na hilo linaloendeklea nchini na kimataifa katika afya zao na za umma.

TANGAZO

# TAARIFA YA VIWANGO VYA TIGO KWA ROBO YA KWANZA JANUARI - MACHI 2020

## Viwango unavyotozwa kwa kadri unavyotumia (Bila Kodi)

**- Malipo ya sauti yamekadiriwa kwenye sekunde iliyo karibu
- Malipo ya data yamekadiriwa kwa shilingi 0.4 kwa kila kilobaiti 10 za data

| VIWANGO VYA NDANI | |
|---|---|
| **Aina za simu** | **Bei (Sh/Dk)** |
| Tigo-Tigo (Viwango ni vya muda wowote) | 65 |
| Tigo-Mitandao mingine (Viwango ni vya muda wowote) | 65 |

| VIWANGO VYA KIMATAIFA | | |
|---|---|---|
| **Aina za simu (Kanda/Makundi)** | **Bei (Sh/Dk)** | **Nchi** |
| Kundi A | 739 | Kenya,Angola, Afrika Kusini, Nigeria, Botswana, Ghana, Ethiopia |
| Kundi B | 739 | Lebanon, Israel, Hispania, U.A.E, Uingereza (simu za kiganjani), Uingereza (Simu za mezani) |
| Kundi C | 1825 | Nchi nyinginezo |
| Kundi D | 1825 | Cuba, DRC, Burundi, Zimbabwe, Msumbiji, Uswisi, Malawi, Zambia |
| Kundi E | 14342 | Mitandao yote ya satelaiti |
| Kundi F | 1304 | Australia, Nepal, Uturuki, Urusi, Visiwa vya Comoro, Uganda, Rwanda, Ufaransa, Denmark, Italy, Oman, Ujerumani |
| Kundi G | 869 | Sweden, Hong Kong, Pakistan, Yemen, Ufilipino, Saudi Arabia, Uholanzi, Japan, Malaysia, Norway, Ireland |
| Kundi Z | 522 | China, India, Marekani, Canada |

| VIWANGO VYA SMS | |
|---|---|
| **Aina za SMS** | **Bei (Sh/SMS)** |
| SMS za kitaifa | 51 |
| SMS za kimataifa | 156 |

| DATA TARIFFS | |
|---|---|
| **Intaneti** | **Bei (Sh)** |
| Data kwa MB | 29 |

## VIWANGO VYA VIFURUSHI VYA DAKIKA, INTANETI NA SMS (Na Kodi)

Mitandao yote

| Bei | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda | Ziada |
|---|---|---|---|---|---|
| 500 | 25 | 50 | 0 | Saa 24 | N/A |
| 1000 | 85 | 50 | 0 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | 240 | 50 | 0 | Saa 24 | N/A |
| 1000 | 30 | 20 | 350 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | 120 | 20 | 1024 | Saa 24 | N/A |
| 3000 | 220 | 100 | 0 | Siku 7 | N/A |
| 5000 | 500 | 100 | 0 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 1100 | 100 | 0 | Siku 7 | N/A |
| 15000 | 1700 | 100 | 0 | Siku 7 | N/A |
| 3000 | 120 | 100 | 2048 | Siku 7 | N/A |
| 5000 | 250 | 100 | 3584 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 550 | 100 | 8192 | Siku 7 | N/A |
| 15000 | 950 | 100 | 13312 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 1150 | 500 | 0 | Siku 30 | N/A |
| 20000 | 2600 | 500 | 0 | Siku 30 | N/A |
| 30000 | 3900 | 500 | 0 | Siku 30 | N/A |
| 50000 | 6900 | 500 | 0 | Siku 30 | N/A |
| 10000 | 550 | 500 | 6144 | Siku 30 | N/A |
| 20000 | 1500 | 500 | 13312 | Siku 30 | N/A |
| 30000 | 2400 | 500 | 21504 | Siku 30 | N/A |
| 50000 | 4000 | 500 | 35840 | Siku 30 | N/A |

Kimataifa

| Bei | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1000 | Nchi nyinginezo duniani - Dk 20 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Nchi za Afrika - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Nchi za Kiarabu - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Nchi nyinginezo duniani - Dk 70 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Nchi za Afrika - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Nchi za Kiarabu - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Nchi nyinginezo duniani - Dk 250 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Nchi za Afrika - Dk 20 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Nchi za Kiarabu - Dk 18 | 0 | 0 | Siku 30 |

***Nchi nyingine Duniani:** India, Marekani, Canada, China, Hong Kong, Ujerumani & Uingereza
***Afrika:** Afrika ya Mashariki, Afrika ya Kusini & Afrika ya Magharibi
***Uarabuni:** UAE, Yemen, Pakistan, Saudia Arabia, Qatar, Lebanon

SMS

| Bei | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 500 | 0 | 300 | 0 | Saa 24 |
| 1000 | 0 | 1000 | 0 | Siku 7 |
| 1500 | 0 | 1000 | 0 | Siku 30 |
| 2000 | 0 | 3000 | 0 | Siku 30 |

Bila Kikomo

| Bei | Jumla ya Dakika | SMS | MB |
|---|---|---|---|
| 500 | 8 | 0 | 0 |
| 1000 | 20 | 0 | 0 |
| 1000 | 12 | 50 | 5 |
| 1000 | 25 | 50 | 5 |
| 2000 | 45 | 0 | 0 |
| 5000 | 135 | 100 | 25 |

INTANETI

| Bei | MB | Muda | Ziada |
|---|---|---|---|
| 500 | 100 | Saa 24 | N/A |
| 1000 | 750 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | 3072 | Saa 24 | N/A |
| 3000 | 3072 | Siku 7 | N/A |
| 5000 | 6144 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 13312 | Siku 7 | N/A |
| 15000 | 22528 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 10240 | Siku 30 | N/A |
| 20000 | 22528 | Siku 30 | N/A |
| 30000 | 34816 | Siku 30 | N/A |
| 50000 | 61440 | Siku 30 | N/A |

SOCIAL

| Bei | MB | Muda | Ziada |
|---|---|---|---|
| 1000 | WhatsApp+Facebook - Mb 1024 | Saa 24 | N/A |
| 1500 | WhatsApp+Facebook+Instagram+Twitter - Mb 2048 | Saa 24 | N/A |
| 1000 | WhatsApp+Instagram - Mb 1024 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | WhatsApp+Facebook - Gb 3 | Saa 7 | N/A |
| 3000 | WhatsApp+Facebook+Instagram+Twitter - Gb 6 | Saa 7 | N/A |
| 2000 | WhatsApp+Instagram - Gb 3 | Saa 7 | N/A |
| 15000 | Home Internet - Gb 12 | Siku 7 | N/A |
| 25000 | Home Internet - Gb 20 | Siku 7 | Gb 20 Usiku |
| 35000 | Home Internet - Gb 30 | Siku 7 | Gb 30 Usiku |
| 5000 | WhatsApp+Facebook - Gb 8 | Siku 30 | N/A |
| 8000 | WhatsApp+Facebook+Instagram+Twitter - Gb 16 | Siku 30 | N/A |
| 5000 | WhatsApp+Instagram - Gb 8 | Siku 30 | N/A |
| 50000 | Home Internet - Gb 30 | Siku 30 | Gb 30 usiku + dk 150 |
| 85000 | Home Internet - Gb 50 | Siku 30 | Gb 50 usiku + dk 300 |
| 120000 | Home Internet - Gb 100 | Siku 30 | Gb 100 usiku + dk 400 |

VIDEO

| Bei | MB | Muda | Ziada |
|---|---|---|---|
| 500 | Youtube-Mb 600 | Saa 24 | N/A |
| 1000 | Youtube- Gb 2 | Saa 24 | N/A |
| 1000 | Startimes-Gb 1 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | Startimes-Gb 1.5 | Saa 24 | N/A |
| 1500 | Kwese/iflix-Gb 1 | Saa 24 | N/A |
| 3000 | Kwese/iflix VIP-Gb 1 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | DSTV - Gb 1.5 | Saa 24 | N/A |
| 7000 | Startimes - Gb 6 | Siku 7 | N/A |
| 7000 | Kwese/Iflix - Gb 6 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | Kwese/Iflix - Gb 6 VIP | Siku 7 | N/A |
| 7000 | DSTV -Gb 6 | Siku 7 | N/A |
| 20000 | Startimes - Gb 16 | Siku 30 | N/A |
| 20000 | Kwese/ Iflix -Gb 16 | Siku 30 | N/A |
| 25000 | Kwese/ Iflix -Gb 16 VIP | Siku 30 | N/A |
| 20000 | DSTV -Gb 16 | Siku 30 | N/A |

**MIC TANZANIA PLC,**
Derm Complex, Kiwanja Namba 11, Kitalu 45 A, Barabara ya Bagamoyo
S.L.P 2929, Dar es Salaam, Tanzania.

**www.tigo.co.tz**

tigo

# Mtoto afa kwa kujinyonga akicheza

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

MTOTO wa miaka 11, mkazi wa Kwamatias Wilaya ya Kibaha, anadaiwa kujinyonga kwa shuka hadi kufa wakati akibembea.

Kamanda wa Polisi mkoani Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema taarifa za kifo cha mtoto huyo zilitolewa na baba yake, Yahaya Hussein.

Kamanda Wankyo alieleza tukio hilo lilitokea April 19, majira ya mchana, na kuwa mtoto huyo akiwa na mdogo wake, waliingia kwenye moja ya chumba kwenye nyumba yao na kufunga shuka dirishani kisha kuanza kubembea.

Wankyo alisema wakati wakiendelea na mchezo huo, shuka waliokuwa wakitumia lilijifunga shingoni kwa mtoto huyo na kumbana hadi kukosa pumzi.

Inaelezwa kuwa mdogo wa mtoto huyo, aliposhuhudia hali hiyo alikimbia kutoa taarifa kwa wazazi wake, ambao walimkimbiza kupata matibabu katika Hospitali ya Tumbi, lakini alipofikishwa ilithibitishwa kuwa ameshafariki dunia.




Washindi 5 wa NMB Mastaboda wakionyesha kadi za Pikipiki baada ya kukabidhiwa na Kaimu Afisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa (hayupo pichani) wakati wa hafla iliyofanyiaka jijini Dar es Salaam.

# Wadhamini wa aliyejifanya Prof. Mbarawa watozwa faini

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imewaamuru wadhamini Petro Massawe na Aslam Shoo, kulipa fungu la dhamana la Sh. 700,000 au kwenda jela miezi sita baada ya mshtakiwa Wilfred Massawe, anayedaiwa kujipatia fedha kwa kutumia jina la Waziri wa Maji, Profesa, Makame Mbarawa, kuruka dhamana.

Amri hiyo imetolewa baada ya wadhamini kuiomba mahakama kulipa fungu la dhamana hiyo ili waachiwe huru kutokana na mshtakiwa kuruka dhamana na juhudi za kumtafuta mikoa tofauti kushindikana.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally, kufuatia mshtakiwa huyo kuruka dhamana tangu Desemba 19, 2019.

Awali, Wakili wa Serikali, Janeth Magoho, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri, lakini mshtakiwa ameruka dhamana na upande wa Jamhuri haujaita shahidi.

Hata hivyo, Petro alidai kuwa yeye na mdhamini mwenzake wamefanya juhudi za kumtafuta mshtakiwa wakisaidiana na jeshi la polisi Kisarawe mkoani Pwani, Ifakara mkoani Morogoro na Iringa, lakini wameshindwa kumpata.

"Mheshimiwa hakimu kwa sasa mshtakiwa hapatikani hewani kwa hiyo tunaomba kulipa fungu la dhamana ili tuwe huru na jukumu hili," alidai Massawe.

Alidai kuwa waliingia mkataba na mahakama kuhakikisha kila tarehe ya kesi mshtakiwa anafika mahakamani kusikiliza kesi hiyo, lakini ametoroka na wamemtafuta kuanzia nyumbani kwake bila mafanikio.

Aliiomba mahakama ikubali walipe fungu hilo la dhamana ili wabakie kuwa huru.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa hauna pingamizi na ombi la wadhamini, lakini waendelee kutoa msaada pale watakapohitajika na jeshi la polisi ili kufanikisha kumpata mshtakiwa.

Hakimu Ally alisema kwa kuwa mshtakiwa ameshindwa kufuata masharti ya dhamana tangu Desemba 19, 2019 mahakama yake inamfutia dhamana na inatoa hati ya kukamatwa kwake.

"Mahakama yangu baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, inaamuru wadhamini hao kulipa fungu la dhamana wakishindwa watakwenda jela kutumikia kifungo cha miezi sita, pia waendelee kutoa msaada kwa jeshi la polisi pale watakapohitajika kufanikisha kumpata mshtakiwa," alisema Hakimu Ally. Desemba 19, 2019 Waziri Mbawala alifika mahakamani hapo kwa ajili ya kutoa ushahidi, lakini mshtakiwa hakuwapo na mahakama iliamuru wadhamini kwenda kujieleza na kutoa hati ya kukamatwa mshtakiwa huyo.

Katika kesi ya msingi, Massawe anakabiliwa na mashtaka manne ikiwamo ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, kujifanya yeye ni Profesa Mbarawa kipindi hicho akiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano,

Mashtaka mengine yanayomkabili ni kujitambulisha kwa Waziri Kindamba ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) kuwa ni Profesa Mbarawa.

Katika kesi hiyo namba 3/2017 Massawe anadaiwa Novemba 25, 2016 akiwa maeneo ya Yombo Buza Temeke jijini Dar es Salaam, alijitambulisha kwa Alfred Samson kwamba yeye ni Profesa Makame Mbarawa.

Katika shitaka la pili, inadaiwa Novemba 26, mwaka na mahali hapo, Massawe alijitambulisha kwa Izack Mwawima kuwa yeye ni Profesa Mbarawa.

Inadaiwa mshtakiwa huyo pia alijitambulisha kwa Waziri Kindamba kuwa yeye ni, Profesa Mbarawa.

# Maelfu bodaboda waingia mfumo rasmi wa kifedha

**Na Mwandishi Wetu**

WAENDESHA bobaboda wapatao 4,855 wameanza kutumia mfumo rasmi wa huduma za kifedha baada ya kuunganishwa na huduma ya NMB MastaBoda.

NMB kwa kushirikiana na MasterCard ilizindua huduma ya MastaBoda mwanzoni mwa mwaka jana ikiwa na lengo la kumwezesha mwendesha bodaboda na abiria wake kulipa nauli kwa kutumia simu za mkononi na fedha hizo kwenda moja kwa moja kwenye akaunti ya NMB ya dereva husika.

"Mpaka sasa, bodaboda 4,855 wameshaunganishwa kwenye huduma hii na mpaka mwishoni mwa mwaka huu, tunategemea kuwafikia madereva boda boda zaidi ya 75,000 nchi nzima," Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha, Benedicto Baragomwa, alisema jijini Dar es Salaam jana.

Baragomwa alikuwa akizungumza katika hafla ya makabidhiano ya zawadi kwa washindi watano wa kampeni ya MastaBoda.

Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa kuna waendesha bodaboda zaidi ya milioni mbili nchini, ambao wengi wao bado hawajaingia kwenye mfumo rasmi huku wakiwa hawana akaunti za benki, hivyo jambo hili limekuwa likiwanyima fursa nyingi za kibenki.

"Ili kutoa motisha kwa madereva bodaboda, tuliweka zawadi kwa wale watakao kuwa vinara wa utumiaji wa huduma za kibenki katika kufanikisha malipo ya nauli kwa abiria wao, motisha hizi ni zawadi za pikipiki kwa washindi watano ambao kila mmoja anajipatia pikipiki, simu za mikononi na pia zawadi za fedha taslimu," alisema Baragomwa.

Benki hiyo imeshatoa zawadi kwa zaidi ya wendesha bodaboda 100, ambao wamejishindia fedha taslimu Sh. 50,000 kwa kila mmoja huku wengine 10 wakijishindia simu janja.

"Kikubwa zaidi leo tunatoa zawadi za pikipiki tano aina ya Boxer kwa madereva 5. Hawa wamefanya miamala mingi zaidi kupitia Mastercard QR. Hawa watano ni wale wa kwanza wenye miamala mingi zaidi kwa mwezi," alisema.

Alisema kuna umuhimu kwa jamii kufanya malipo kupitia Mastercard QR hususan kipindi hiki kigumu ambacho dunia nzima inapitia kwenye mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19.

"Ukilipia kwa mfumo huu abiria na dereva wanapunguza uwezekano wa kusambaza ugonjwa kwa kuwa hakuna matumizi ya noti...Tunawasihi Watanzania wote na wafanyabiashara kwa ujumla watumie mfumo huu ambao ni rahisi, salama na wa uhakika pindi wanapotoa ama kulipia huduma," alisema

Naye Meneja Masoko wa MasterCard Afrika Mashariki Teresa Moraa alisema:

"Kupitia ushirikiano wetu na Benki ya NMB, tumefanya jitihada kuzindua Mastercard QR na kampeni ya Mastaboda ili kuwasaidia wafanyabiashara kupokea malipo kwa mfumo wa kidijitali na pia wateja kufanya malipo kwa njia salama, rahisi na kutohitaji kuwa na pesa tasilimu."

# Onyo viwanda kununua chuma chakavu kimagendo

**Na Maulid Mmbaga**

KATIKA kukabiliana biashara ya magendo ya chuma chakavu nchini, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewataka wenye viwanda kufuata sheria, kanuni na taratibu zinazoelekeza ununuzi wa chuma chakavu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana,

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dk. Samuel Gwamaka, aliwaelekeza wenye viwanda kununua chuma chakavu kutoka kwa wafanyabiashara waliosajiliwa na kutambuliwa na Baraza.

"Utafiti wetu unaonesha uhujumu mkubwa wa miundombinu nchini, hali ambayo ilichangia kufunga usafirishaji wa chuma chakavu nje ya nchi.

Kuanzia sasa wenye viwanda wote watalazimika kununua chuma chakavu kutoka kwa wafanyabiashara ambao wamesajiliwa na NEMC ili kulinda miundombinu," alisema Dk. Gwamaka. Dk.. Gwamaka alisema NEMC ilishakutana na wadau na wafanyabiashara wa chuma chakavu ili kupata maoni yao yaliyotumika kutengeneza kanuni mpya za ufanyaji wa biashara ya chuma chakavu za mwaka 2019.

"Kanuni mpya zinawataka wafanyabiashara wa chuma chakavu kuwa na vibali ambavyo vitatolewa na NEMC baada ya kujiridhisha," alisema, na kuongeza kuwa atakayekiuka kanuni na taratibu atachuliwa hatua za kisheria ikiwamo kutaifishwa mzigo wake.

Aalsema vibali vya kukusanya chuma chakavu vinatolewa kwa gharama ya shilingi 50,000, ambapo tozo zake mwaka ni kati ya shilingi milioni 1.5 hadi milioni tano.

Alisema mbali ya kuzuia uharibifu wa miundombinu, zuio hilo liltoa nafasi ya kutafiti namna gani vyuma chakavu visafirishwe nje ya nchi pasipo kuhujumu azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

"Serikali imekuwa ikitekeleza azma ya kujenga uchumi wa kati na Viwanda, hivyo lazima NEMC iunge mkono azma hiyo kwa vitendo kwa kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa chuma chakavu kama sehemu ya malighafi muhimu kwenye viwanda,' alisema Dk. Gwamaka.

Hata hivyo, alisema katika kuhakikisha chuma chakavu kipatikana kwa wingi hnchini, serikali inahamasisha wafanyabiashara wanaoingiza chuma chakavu kutoka nje ya nchi ambayo kila tani moja italipiwa shilingi 7,500 tofauti na wale wanaosafirisha nje watalipa shilingi 30,000 kwa tani moja.



Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Shinyanga, Hussen Mussa, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari mkoani humo, juu ya uokoaji wa fedha Sh. 118,851,957 kutoka kwa vyama vya msingi vya ushirika AMCOS pamoja na SACCOS, fedha za wakulima na wana chama ambazo ni miongoni mwa fedha zilizotafunwa na viongozi wa vyama hivyo, kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020, kuanzia Januari hadi Machi. **PICHA : MARCO MADUHU**

# Masoko yalivyokuza sekta madini

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

WIZARA ya Madini imesema uanzishwaji na usimamizi wa masoko ya madini nchini umeongeza kasi ya ukuaji wa sekta hiyo kutoka asilimia 0.9 hadi 12.6.

Akiwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2020/2021, Waziri wa wizara hiyo, Dotto Biteko, alisema kuwapo kwa masoko na vituo vya ununuzi wa madini kwenye sehemu za uchimbaji kumetatua changamoto ya muda mrefu hasa kwa wachimbaji wadogo kukosa uhakika na bei stahiki.

Alisema kwa kipindi cha kuanzia Machi, 2019 hadi Februari, 2020, kwenye masoko hayo kumeuzwa madini yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni 1 na kuiingizia Serikali mapato kwa kulipa mrabaha na ada ya ukaguzi wa zaidi ya Sh. bilioni 78.

"Masoko haya yameleta mabadiliko makubwa katika sekta ya madini ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa sekta kutoka asilimia 0.9 mwaka 2018 hadi 12.6 mwaka 2019," alisema. Kwa mujibu wa Biteko, masoko hayo yameleta manufaa mengine kwa wananchi ikiwamo kuzalisha fursa za ajira na kuongezeka kwa kipato cha wachimbaji wadogo.

Kuhusu uanzishwaji wa eneo tengefu la Mirerani, alisema kuwapo kwa vifaa vya usalama kumeongeza mapato kutokana na wachimbaji wadogo kutoka zaidi ya Sh. milioni 166 kabla ya kujenga ukuta hadi zaidi ya Sh. bilioni 2.1 baada ya ukuta.

Alisema kasi ya ukuaji wa sekta ya madini ni asilimia 12.6 ikiwa ni nafasi ya pili baada ya ujenzi iliyokua kwa asilimia 14.8. Kuhusu wachimbaji wadogo, alisema kufutwa kwa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na kodi ya zuio kwa wachimbaji wadogo kunapaswa kuungwa mkono "Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini mbalimbali yakiwamo dhahabu, makaa ya mawe, tanzanite na almasi," alisema.

# Waandishi wa habari wapigwa jeki barakoa

**Na Romana Mallya**

MAKUNDI kwenye jamii wakiwamo waandishi wa habari ambao wanaendelea na kazi ya kuhabarisha umma dhidi ya virusi vya corona yametakiwa kuchukua tahadhari zinazotolewa na wataalam wa afya.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Meneja Mauzo wa kampuni ya FMJ Hard Ware, Fredrick Sanga, kwa niaba ya wakurugenzi wake, wakati akikabidhi vitakasa mikono kwa waandishi wa habari ili viwasaidie kwenye kazi zao. "Tunatoa msaada wetu kwa vyombo vya habari kama sehemu ya kuunga mkono jitihada za Serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Corona.

"Tunatambua mchango wa vyombo vya habari katika kuhabarisha umma wa Watanzania katika masuala mbalimbali yanayotokea nchini hususani janga la corona."

Alisema wameamua kuwasaidia waandishi wa habari vitakasa mikono ili viwasaidie wawapo kwenye majukumu yao kujikinga na maambukizi ya virusi hivyo.

"Tunaamini wadau wengine watajitokeza kuiunga mkono Serikali kwa kutoa misaada ambayo itaongeza nguvu kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa corona," alisema.

Pia Sanga alitumia fursa hiyo kuwakumbusha wafanyabiashara hususan wanaojishughulisha na uuzaji wa vifaa vya ujenzi na mafundi, wazingatie tahadhari zote za kujilinda na corona zinazotolewa na serikali.

# Ahoji uhalali trafiki kupiga picha magari mafichoni

MBUNGE wa Jang'ombe (CCM), Ali Hassan King (pichani), amehoji uhalali wa askari wa usalama barabarani, maarufu trafiki, kupiga picha magari yenye mwendokasi kwa kificho.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alihoji: "Je, ni sahihi kwa askari wa usalama barabarani kupiga picha magari yenye mwendokasi eneo moja kwa kificho na askari mwingine kukamata magari haya eneo tofauti na tukio?"

Katika majibu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yaliyotolewa kwa swali hilo, ilisema Jeshi la Polisi pamoja na wajibu wake wa kulinda maisha na mali ya wananchi, pia linao wajibu wa kusimamia sheria na kuhakikisha kila mtu anatii sheria bila shuruti.

"Katika utendaji kazi wa kuhakikisha kuwa dhana ya utii wa sheria bila shuruti inatekelezwa, Jeshi la Polisi hutumia mbinu mbalimbali ili kubaini tabia za madereva wawapo barabarani na uhiari wa kutii sheria za barabarani," ilisema.

Ilibainisha kuwa kupiga picha gari iliyozidisha mwendo katika eneo moja, tena ambalo askari huwa amejificha, ni mojawapo ya mbinu za kuhakikisha madereva wanatii sheria bila shuruti.

"Hivyo madereva wanaozidisha mwendo, hupigwa picha na kisha kuituma kwa askari walio mbele ili kumkamata kwani askari mwenye 'speed', kamera huwa ni vigumu kupiga picha na kisha kulikamata gari hilo kwa wakati huo huo," ilisema.



# Gesi iliyogunduliwa yafikia futi tril. 57



BUNGE limeelezwa kuwa hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu, gesi asilia iliyogunduliwa nchi kavu na baharini ilikuwa futi za ujazo trilioni 57.54.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Wizara ya Nishati ilipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Shamsia Mtamba (pichani).

Katika swali lake, mbunge huyo alisema mikoa ya kusini ndiyo inayotoa gesi kwa wingi kwa sasa, na akahoji mkakati wa serikali kujenga kituo cha kutoa mafunzo kuhusu rasilimali hiyo ya taifa.

"Je, ni lini serikali itajenga chuo cha kutoa mafunzo juu ya rasilimali hiyo na mafuta ili wananchi wa Mtwara na Lindi wapate fursa zaidi ya elimu ya gesi na mafuta?" alihoji.

Katika majibu yake, wizara hiyo ilisema ugunduzi wa gesi hiyo umefanyika kuanzia mwaka 2010 katika vitalu namba 1,2,3 na 4 vilivyopo katika maeneo ya kina kirefu cha bahari (deep sea) ambapo kuna futi za ujazo 47.27.

"Matumizi ya gesi asilia iliyogunduliwa Songo Songo na Mnazi Bay yalianza mwaka 2004 na mwaka 2006 sawia," ilisema. Ilisema kuwa kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Kampuni za Kimataifa za Mafuta na Gesi (IOC's) na Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) hutoa mafunzo kwa Watanzania wenye sifa, wanafunzi na wakufunzi ili kujenga uwezo wa kitaalamu kwa Watanzania na kukidhi mahitaji ya wataalamu katika soko la ndani.


"Hadi sasa, vyuo vya VETA katika mikoa ya Lindi na Mtwara hutoa mafunzo ya kiufundi yanayohusu masuala ya mafuta na gesi asilia,"ilisema.

Ilieleza kuwa hadi sasa, zaidi ya wahitimu 350 wa VETA wamepatiwa vyeti vinavyotambuliwa kimataifa ili kuwawezesha kupata ajira katika kampuni za kimataifa za mafuta na gesi asilia nchini na nje ya nchi.

"Jitihada hizi zimegharimu takribani Dola za Marekani milioni nne. Pamoja na kufundisha vijana kupitia VETA, TPDC kwa kushirikiana na Kampuni ya Gesi na Mafuta ya Kimataifa (IOC's) hutoa mafunzo kwa wajasiriamaliili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma katika shughuli na miradi ya mafuta na gesi asilia," ilisema.

Wizara hiyo pia ilisema hadi sasa wajasiriamali 195 katika mikoa ya Lindi na Mtwara wameshapatiwa mafunzo hayo.

"Serikali kupitia TPDC imefungua klabu 32 za mafuta na gesi katika shule za sekondari za Lindi na Mtwara kwa lengo la kutoa elimu inayohusu tasnia ya mafuta na gesi asilia pamoja na namna inavyoweza kuwanufaisha kupitia fursa zinazotengenezwa na tasnia hii katika maeneo yao," ilisema.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA



# Uchimbaji madini ya Niobium kuanza

WIZARA ya Madini imesema inatarajia kutoa mapendekezo ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa uchimbaji madini ya Niobium chini ya Kampuni ya Panda Hill.

Ilitoa kauli hiyo jana bungeni katika majibu yake kwa Mbunge wa Mbeya Vijijini (CCM), Oran Njeza (pichani juu) ambaye alihoji ni lini uzalishaji wa madini hayo utaanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Katika majibu yake, wizara hiyo ilisema kampuni hiyo ina ubia na kampuni ya Cradle Resources Limited asilimia 50 na Tremont Investments asilimia 50.

"Kampuni hiyo inamiliki leseni tatu za uchimbaji wa kati wa madini ML 237/2006, ML 238/2006 na ML 239/2006 zilizotolewa tarehe 16 Novemba 2006 zikiwa na kilomita za eneo la mraba 22.1," ilisema.

Ilieleza kuwa mradi utahusisha uchimbaji wa madini ya Niobium ambayo yataongezewa thamani kwa kuchanganywa na madini ya chuma na kuwa Ferro-Niobium, zao ambalo litauzwa kwa wanunuzi mbalimbali waliopo Ulaya, Asia na Amerika ya Kaskazini.

"Mwekezaji ameshafanya upembuzi yakinifu (Feasibility Study) uliokamilika mwaka 2016 na kujiridhisha uwapo wa mashapo ya kutosha utakaowezesha uhai wa mgodi kwa takriban miaka 30,"ilisema.

Hata hivyo, ilisema kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2017, mwekezaji alilazimika kupitia upya na kurekebisha taarifa ya upembuzi yakinifu ili kuzingatia viwango vipya vya mrabaha, kodi na hisa za serikali.

"Hivyo, mwekezaji amewasilisha andiko la mradi la kuomba ufafanuzi wa vipengele mbalimbali vya sheria na kutoa mapendekezo yake juu ya utekelezaji wa mradi huo, pamoja na suala la fidia ya ardhi kwa Gereza la Mbeya ambalo linatakiwa kuhamishwa ili kupisha mradi," ilisema.

Ilibainisha kuwa baada ya kupokea andiko hilo, hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwamo majadiliano na mwekezaji.

ama

ALHAMISI APRILI 23, 2020

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

**Wakala Misitu kuanzisha kiwanda mkaa mbadala**



Ukurasa 13

Wasomi: Silaha ya corona sasa ni mlo, usingizi kamili



Ukurasa 14

**Nguva ni binadamu au samaki?**

AFYA

# Hatua kubwa mkoa Kigoma kliniki ya mume, mke, mtoto

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MKOA wa Kigoma kwa miaka miwili mfululizo, umeingia katika hesabu ya maendeleo ya kinababa kushiriki katika masuala ya afya ya uzazi, katika eneo la kliniki ya baba, mama na mtoto.

Awali Kigoma, ushiriki wa wanaume ulikuwa mdogo sana, kwani ulikuwa chini ya asilimia 20, kutokana na kundi hilo kuona afya ya uzazi inamuhusu mwanamke pekee.

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa Mkoa, Ernest Teyumwete, anasema takwimu za mwaka juzi zinataja ushiriki wa kinababa ulikuwa asilimia 56, lakini hadio kufika mwaka jana, zimeongezeka hadi asilimia 79.

Teyumwete anasema, mafanikio hayo ni matokeo ya mkakati wa kuongeza uelimishaji wa kundi hilo, hata likatambua wanawajibika katika afya ya uzazi, hususani kujua maendeleo ya wenza kipindi cha ujauzito. Anasema, awali kliniki zilikuwa si rafiki kwa wanaume, kwa huduma hiyo kuchukua muda mrefu, hali inayosababisha mahudhurio duni ya wanaume, hata wakaamua kujikita katika mengine.

"Hasa katika kipindi cha kwanza cha kliniki ya ujauzito, kuna mambo mengi ambayo wote wanapaswa kufahamu, lakini kinababa wengi wanadhani ni upimaji wa ugonjwa wa Virusi vya Ukimwi (VVU) tu, "anasema .

Maoni yake ni pindi wanajinsia hao watashiriki na kupata elimu ya masuala ya uzazi, ni nyenzo inayosaidia kutambua taarifa sahihi za ujauzito, utambuzi wa dalili za hatari inayopunguza matatizo yanayosababishwa na ujauzito.

### KWA NINI KLINIKI?

Kwa mujibu wa Mratibu wa Afya ya Uzazi, kabla ya mwaka 2005 mwanamke mjamzito alishauriwa angalau kuhudhuria kiliniki mara nne kabla ya kujifungua, lakini sasa kutokana na utafiti mbalimbali wa afya, mjamzito anatakiwa ahudhurie mara nane.



Baadhi ya wanaume wa Manipaa ya Kigoma Ujiji, wakiwa kliniki na wenza wao. **PICHA: PENDO THOMAS**

> **"Hasa katika kipindi cha kwanza cha kliniki ya ujauzito, kuna mambo mengi ambayo wote wanapaswa kufahamu...**

Inaelezwa, endapo mwanamke atahudhuria kliniki akiwa na ujauzito chini ya wiki 12, itamsaidia utambuzi wa matatizo ya ujauzito kama malaria na atatumia tiba na kinga, lakini anaposhindwa kufika anaikosa nafasi hiyo.

Pia, anasema ni fursa inayosaidia kutambua magonjwa yanayosababishwa na kujamiiana kama vile kaswende, kisonono, fangasi na matatizo ya uzazi yanayoifanya mimba kutoka au ugumba kwa mwanamke .

Vilevile ni magonjwa yanayosababisha mtoto aliyeko tumboni akazaliwa na kasoro za kibinadamu kama vile kutoona, ubongo na ulemavu mwingineo.

### KIGOMA UJIJI

Takwimu za Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, zinaonyesha mwanga wa mafanikio, kwa kuwaelimisha wanaume kutambua wajibu wao wa kushiriki kliniki za uzazi.

Mratibu Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto, katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, Bernadeta Peter, anasema mwaka 2017 kulikuwapo jumla ya wanaume 74, 82 sawa na asilimia 90.8 waliohudhuria kliniki za wanaume na mwaka uliofuata, waliongezeka hadi 8,519 (98.3%) na mwaka jana ilikuwa asilimia 96.

Anaeleza mafanikio hayo, ni kutokana na mikakati waliojiwekea kutumia makundi mbalimbali katika kuelimisha wanaume kuongeza ushiriki katika masuala ya afya ya uzazi.

Bernadeta anasema, kwa sasa wanatumia viongozi wa jamii kusaidia uhamasishaji wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii, ambao huwaelimisha kinamama, ili nao waende kuwafundisha waume zao wajibu wa kuhudhuria kliniki na wake zao.

Hata hivyo, anadokeza kuwapo changamoto za waliopewa ujauzito kutoka waume wasio wao, hali inakuwa mtihani kufika nao kliniki, ambayo pia ndio chanzo cha mgogoro katika jamii.

Aidha, Bernadeta ana lingine la wanaume kuwa na majukumu ya safari za kikazi, hata wanakuwa mbali na familia, ikiwamo mahudhurio ya kliiniki za wake ujauzito unaowahusu na la mwisho ni mfumo dume uliopo.

Gazeti Nipashe ilimhoji, David Daniel, mkazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji, kuhusu ushirika wa kliniki na ufafanuzi wake: "Nakuja kliniki ili nipate maelekezo ya watalamu kuhusu mtoto ajaye na kuwa na kufahamu maendeleo yake, hivyo sioni kama ni usumbufu kukaa hapa kliniki kupata elimu hiyo.'

Pia, Daniel anawataka wanaume wenzake kutoa kipaumbele kwa suala hilo, pasipo kupuuzia kutokana na kuwa na faida kwa familia zao na kumlinda mtoto aliyeko tumboni.

Sophia Staslaus, anaunga mkono kuwa baada ya kuelimishwa ushiriki wa mwanaume katika kliniki ya baba mama na mtoto, alienda kumueleza mume wake dhana itakayowapa mtoto mwenye afya njema ushiriki wao kwa pamoja, akiainisha hali ilivyokuwa:

"Mwanzo ilikuwa ngumu kumuelewesha, lakini kutokana na elimu niliyopatiwa na wataalamu wa afya, niliweza kuongea nae na baadae alinielewa na akaanza kutekeleza."

MAZINGIRA

# Wakala Misitu kuanzisha kiwanda mkaa mbadala kunusuru miti yake

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

• Wauza mkaa, wachimba madini balaa

UCHOMAJI mkaa na matumizi ya miti kwa wachimba madini wadogo, tayari umeshaleta madhara ya kimazingira, dhidi ya kampeni ya kuifanya Tanzania kuwa ya kijani, wilaya za Kahama na Ushetu, mkoani Shinyanga,

Ushetu kuko juu kwa suala la miti kukatwa na kisha kutumika kuchoma tumbaku. Pia, inatajwa kuchangia uharibifu wa mazingira ambayo athari yake ya moja kwa moja ni kupungua mvua, tofauti na ilivyokuwa nyuma.

Wilaya jirani ya Kahama, kwa sasa ina uharibifu mkubwa wa mazingira unaosababishwa na mambo mbalimbali, ikiwamo shughuli za kibinadamu zinazofanyika ndani ya misitu na mapori yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi.

Msitu wa Mkweni uliopo Kahama, kwa mujibu Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), tayari miti yake imeshapungua na shughuli za uchomaji mkaa unaoendeshwa mahali hapo, hali inayochangia kuwapo changamoto zinazohusu uharibifu wa mazingira.

**TFS KAHAMA**

Juma Ally, ni Meneja wa TFS, wilayani Kahama, anasema wameanzisha mradi wa kuzalisha mkaa mbadala uliopewa jina la 'Briquette Production Project' wenye thamani ya Sh. milioni 15 kutatua changamoto ya uvunaji misitu na uchomaji mkaa.

Anasema wilaya hiyo ina misitu minne, akiutaja Mkweni unaosimamiwa na TFS, una jumla ya hekta 15,744. Misitu mingine ni Usumbwa, Mpunze na Ushetu-Ubagwe, zote zinasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.

Meneja huyo wa TFS, anasema ni hali iliyochangia mavuno ya mazao ya msitu huo, kuwa katika kiwango cha chini, ikivunwa kiholela.

Anasema hatua ya serikali sasa, imeweka mikakati ya kuichukua misitu hiyo inayomilikiwa na Halmashauri ya Ushetu, ili iwe chini ya TFS kwa ni ya kuwadhibiti wanaovuna holela mazao ya misitu na uchomaji mkaa kiholela.

Pia, anataja malengo ya mradi ni kufikisha hatua iwe na uwezo wa kuzalisha mkaa mbadala zaidi ya tani tatu (kilo 3,000) na watahakikisha kila mwananchi mkazi wilayani, anaupata mkaa, ili kupunguza ukataji kiholela kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Aidha, Ally anasema ni mkaa huo utakaokuwa na uwezo wa kudumu ndani ya jiko kwa saa nne tofauti na mkaa unatokana na mazao ya misitu, unaodumu jikoni kwa wastani wa saa moja na mpaka sasa wameshazalisha tani moja ya mkaa huo.

"Kama tunaweza kuwekeza kwenye madini kwa zaidi ya Sh. milioni 100 hadi 300 kwa kununua makabrasha na kusaga mawe ya dhahabu, basi tunaweza kuwekeza kwenye utengenezaji mkaa mbadala na kupambana na uvunaji huu holela ambao uko juu kwenye wilaya yetu," anafafanua Ally.

Anasema, ni mkakati unaotarajiwa kusaidia kupunguza uvunaji kwenye misitu inayomilikiwa na halmashauri; Usumbwa, Mpunze na Ushetu-Ubagwe kwa zaidi ya nusu ya matumizi ya sasa.

Hata hivyo, Ally anavitaka vikundi vya vijana, kinamama na wenye ulemavu wajitokeze kujifunza namna ya utengenezaji mkaa huo bora na wa kisasa, wakaanzisha viwanda vidogo.

Kwa mujibu wa meneja huyo, mtaji unaohitajika kuanzisha kiwanda aina hiyo, ni kati ya Sh. milioni nane hadi 15, kulingana na ukubwa wa mashine inayohitajiwa kutumika.



Magunia ya mkaa yaliyokamatwa na Wakala wa Huduma za Misitu, katika operesheni ya kukamata mazao yatokanayo na misitu. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

> "Kikundi cha Corido, hutumia malighafi ya pumba za mpunga, randa za mbao na maganda ya karanga, katika kutengeneza mkaa wao mbadala, ambao kimsingi ni mzuri majumbani.



Meneja wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), wilayani Kahama, Juma Ally, akionyesha mashine inayotengeneza mkaa mbadala wa kupambana na uvunaji na uchomaji mkaa holela.

**KIKUNDI CARIDO**

Kikundi cha Kahama Corido kipo katika Mji wa Kahama ambacho kilianzishwa na TFS miaka miwili iyopita, lengo ni kupambana na uharibifu wa mazingira na kulinga mazao ya misitu.

Kikundi cha Corido, hutumia malighafi ya pumba za mpunga, randa za mbao na maganda ya karanga, katika kutengeneza mkaa wao mbadala, ambao kimsingi ni mzuri majumbani.

Boniface Chacha ni Ofisa Masoko wa Shirika Kahama Corido, anasema kikundi chao kina watumishi watano wanakihudumia na wameweza kutanua wigo wa ajira kwa makundi mbalimbali ya vijana mjini Kahama.

Anasema kuwa, kazi kubwa ya uzalishaji mkaa huo hufanyika katika kipindi cha kiangazi, jua linakuwa kali hata kuwezesha kukausha mkaa huo, ikiwa ndio mbinu kuu wanayotumia katika kipindi kilichopo hawajapata vifaa mbadala kwa ajili ya kukausha mkaa wanaouandaa.

Chacha ana ushauri kwamba, kiwanda kama chao kinaweza kukua, endapo serikali itawazuia watu wanaouza mkaa mitaani, ambao ndio chanzo cha uharibifu wa misitu nchini, hali ambayo ingeleta mbadala wa mafanikio hata wakamudu soko lililopo.

Pia, anataka lingine kuwa tozo kubwa ya kodi kutoka katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), huku wanatumia malighafi isiyotokana na misitu.

Hadi sasa wamiliki hao wanalalamika kiwanda kinazalisha mkaa kidogo kulinganisha na mahitaji ya wakazi wa mji wa Kahama na wenye kiwanda hicho wanaamini elimu sahihi ikitolewa kwa wananchi kuhusu matumizi ya mkaa, itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matumizi ya mkaa utokanao na misitu.

**WANAVIKUNDI**

Rose Godfrey, mkazi wa Nyakato Kahama, ana ushauri ili TFS ifanikiwe kupambana na uvunaji misitu na uchomaji mkaa kiholela kwenye mradi huo, ni vyema wakawekeza nguvu katika kuwafundisha vijana namna ya utengenezaji mkaa mbadala.

Anasema, mtaani kuna vijana wengi wasio na ajira ambao wanapopatiwa elimu sahihi, wanaweza kuungana wakatengeneza viwanda vingi vya mkaa, hata kutosheleza mahitaji ya wilaya Kahama na jirani.

Salvatory Shija, ana maoni kwamba Halmashauri za wilaya Msalala, Ushetu na Kahama Mjini, zina vikundi vinavyowezesha mikopo rahisi na endapo vitapatiwa elimu, vitakuwa na uwezo wa kununua mashine hiyo na kuanza kazi ya kuzalisha mkaa mbadala.

AFYA

# Wasomi: Silaha ya corona sasa ni mlo, usingizi kamili

**Na Jackson Paulo**

• Kasi inafuata majumbani; dawa bado, mashine kupumulia haisaidii



Cameron Kyle-Sidell: Kimbilio la mashine za kupumulia hazisaidii kwa asilimia 80.




Marc Lipsitch wa Chuo Kikuu Havard: Corona itafika asilimia 40 hadi 70 duniani.

MAAMBUKIZI ya virusi vya corona yanazidi kushika kasi na hofu inazidi katika jamii.

Mtaalamu bingwa wa masuala ya virusi kutoka Chuo Kikuu cha Havard nchini Marekani, Marc Lipsitch, anataja ni asilimia 40 hadi 70 ya watu duniani wako hatarini kuambukizwa virusi vya corona na kati yao asilimia moja, huenda watapoteza maisha.

Nchini Uingereza, mshauri wa sayansi serikalini, Rupert Shute, anasema asilimia 80 ya wakazi nchini humo huenda wataishia kupata virusi hivyo hata wakikaa majumbani.

Hayo yanakumbusha wajibu wa kila mmoja kufahamu rasmi yuko vitani kushindana na maambukizi. Hapo inakuja haja ya kuwapo silaha mbadala au ya ziada.

Kwa kawaida, mgonjwa wa corona anapougua na kufikishwa hospitalini, hakuna dawa maalum ya kuangamiza virusi. Wanachofanya madaktari, ni kudhibiti dalili za ugonjwa.

Pia, aliye mahututi anapohamishiwa Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU), msaada mkubwa anaopewa ni katika kupumua.

Hata hivyo, hali ya kushangaza takwimu za karibuni zinaonyesha mashine za kusaidia kupumua (ventilators) zimeshindwa kusaidia kuokoa maisha kwa namna iliyodhaniwa.

Uingereza, utafiti ulihusisha wagonjwa 98 wa corona waliowekewa mashine za kusaidia kupumua, theluthi mbili (67%) walifariki. Hiyo ni ripoti mpya ya Kituo cha Taifa cha Ukaguzi na Utafiti wa Kitengo cha Uangalizi Maalum (ICNARC).

Nchini Marekani, jijini New York kulikoathirika sana na virusi, asilimia 80 ya wagonjwa waliowekewa mashine za kusaidia kupumua walifariki.

China katika mji wa Wuhan, ambako corona ilianzia, watafiti wanaripoti kati ya wagonjwa 37 waliokuwa taabani hadi kuhamishiwa ICU kuwekewa mashine ya kusaidia kupumua, 30 (81%) walifariki ndani ya mwezi mmoja.

Utafiti mwingine huko Seattle Marekani, kati ya wagonjwa saba (umri zaidi ya miaka 70) waliowekewa mashine, mmoja tu ndiye aliyepona na mataifa mengine hali inafanana. Daktari wa majeruhi wa New York, Cameron Kyle-Sidell, anapinga mashine za kusaidia kupumua kwa mgonjwa wa corona.

Ni hali inayowafanya madaktari kwingineko duniani kuhamia mbadala kuwaokoa wagonjwa kwa kuwaongezea Oksijeni kwenye damu kupitia barakoa 'mask' maalum ya na si mashine hizo.

### MAANA YAKE?

Hapo kuna maana, hata kwa mwenye uchumi bora, hospitali pekee haitoshi kumuokoa maisha.

Wapo wanaodhani upungufu wa mashine za kusaidia kupumua katika nchi za Afrika ni janga kwa sasa, lakini ukweli uko katika haja ya kubadili mtazamo kupambana na virusi kwa njia mbadala ambayo ni 'kinga yako ya mwili'.

> **Inawezekana maambukizi ya virusi vya corona yanapomkuta mtu wakati mwili wake ni imara, haonyeshi dalili yoyote au anapokutwa na dallili ya kawaida, anakuwa jirani na kupata.**

Kukabili corona ni vita inayohusisha majeshi ya aina mbili; virusi na kinga ya mwili. Hivyo, ushindi wake unategemea jeshi ambalo ni imara zaidi kati ya virusi na kinga ya mwili.

Kwakuwa kusambaa virusi kunaelezwa inashika kasi ya kusambaa duniani ikiwamo Tanzania, njia bora ya kukabili ni kuliweka jeshi la kinga ya mwili utayari kwa mapambano.

### INAKABILIWA VIPI?

Kunatajwa umuhimu wa kula vyakula vinavyosaidia kuimarisha kinga ya mwili kwa kuhusisha chembehai, mishipa na protini, kuweka michakato mwilini ya kupambana na vimelea kama virusi, bakteria na vingine vya kigeni,vinavyosababisha maambukizo au magonjwa.

Hapo kuna kuhusisha vyakula vya aina fulani kwenye lishe kupambana na magonjwa. Mtu anapaswa kupata mlo unaosaidia kuimarisha kinga mwilini na kuepuka vyakula au hali inayodhoofisha kinga ya mwili. Vifutavyo ni muhimu:

### MATUNDA & MBOGA

Ni muhimu kuimarisha kinga ya mwili. Mboga kama spinachi ina virutubisho vingi muhimu kama vitamin C na E, zinazongezea mwili kinga.

Matunda nayo yana utajiri mkubwa wa vitamini C; yanatajwa machungwa, limao, ndimu, embe, nanasi na tikiti maji, ndizi na parachichi.

### TANGAWIZI, VITUNGUU SWAUMU

Utafiti unaonyesha tangawizi inasaidia kuimarisha kinga mwilini, japo wanasayansi wanahitaji utafiti zaidi kuthibitisha uwezo wa kuzuia magonjwa.

Majumbani hutumika kuzuia homa za baridi na na magonjwa mengine. Kuna utafiti unataja vitunguu swaumu zinapunguza hatari ya kupata homa.

### CHAI KIJANI, ZABIBU

Chai ya kijani ina kiasi kidogo cha kafeini, kwa hivyo inaweza kuwa mbadala wa chai nyeusi au kahawa. Inaimarisha kinga na kupunguza maambukizi ya mafua, lehemu (cholesterol).

Pia, inatajwa kukabili magonjwa ya moyo, kisukari na inapungua uzito mwilini, ikiongeza uwezo wa kumbukumbu za mwanadamu.

Zabibu nayo inalinda njia za kupumua na kupunguza maambukizi ya maradhi kwa njia za upumuaji au homa ya kawaida.

### USINGIZI & UNYWAJI MAJI

Kupata muda wa kutosha kulala ni silaha kubwa. Mwili unahitaji kupumzishwa kwa walau saa saba hadi tisa kwa siku, tena kwa utulivu unaowezesha mwili kujiweka sawa na unajiimarisha. Fursa hiyo inapokosekana, ni uharibifu wa kinga mwilini.

Maji pia, inachukua asilimia 60 ya mwili wa binadamu, hivyo ni wajibu kunywa maji ya kutosha kila siku, kuufanya mwili ujiendeshe vizuri. Chembehai nazo zinahitaji mazingira yenye maji ya kutosha, zifanye kazi.

### MAZOEZI

Mazoezi ni muhimu sana kwa afya na kinga ya mwili, hasa kwa mtu mnene. Takwimu za Shirika la Huduma ya Afya Uingereza (NHS), zinaonyesha asilimia 38 ya waliolazwa katika Chumba cha Uangalizi Maalumu (ICU), kutokana na virusi vya corona ni watu wanene na kati yao, asilimia 55 walifariki.

Wenye unene uliopitiliza na umri zaidi ya miaka 60, nao idadi ya vifo vyao viko juu .

Hata hivyo, tahadhari iliyoko ni mazoezi kuzidi kiasi yanashusha kinga ya mwili.

### AFYA AKILI

Afya ya akili ina sehemu kubwa katika kinga ya mwili. Sayansi inaonyesha, mwenye msongo wa mawazo au hofu, kinga yake inashuka na mtu anapokuwa katika utulivu, kinga inakuwa juu.

Inawezekana maambukizi ya virusi vya corona yanapomkuta mtu wakati mwili wake ni imara, haonyeshi dalili yoyote au anapokutwa na dallili ya kawaida, anakuwa jirani na kupata.

Hofu au kukata tamaa katikati ya mapambano dhidi ya corona, virusi vinaweza kumshinda mgonjwa.

### VYA KUEPUKA

Katika zama za mlipuko wa virusi vya corona, mtu anapaswa awe kando na mambo au mtindo wa maisha unaomuweka hatarini kuugua au kupoteza maisha, anapoambukizwa.

Mambo ya kuepuka inajumuisha vyakula vinavyopikwa haraka, matumizi makubwa ya sukari, pombe na tumbaku.

Ni wakati wa kuwa na afya nzuri kadri inavyowezekana na kuishi kwa tahadhari kubwa kuepuka maambukizi au kuwaambukiza wengine, pamoja na vigezo rasmi vya tahadhari kutoka serikalini.

***Makala inatokana na taarifa rasmi ya kimataifa na mwandishi anapatikana kwa anwani ya barua pepe: jacpole@gmail.com***

MAZINGIRA

# Nguva ni binadamu au samaki?

## • Fahamu maisha yake yalivyo ndani ya maji

**Na Tuntule Swebe**



Nguva katika mwonekano tofauti, mojawapo akiwa ameshikiliwa na wavuvi amekufa. **PICHA ZOTE : MTANDAO**

NGUVA ni binadamu au samaki? Ni swali ambalo Nipashe lililiweka kwa umma na ikawa gumu kupata ufafanuzi wa moja kwa mmoja.

Mchangiaji mmoja alisema, ni samaki, japo alishindwa kutetea jibu, kwani amegawanyika, sehemu ya juu kama binadamu na chini samaki, sasa kulikoni jibu lake kuangukia upande mmoja?

Mwingine akaingilia kati kunyoosha jibu, kwamba nguva ni samaki, kwa sababu anaishi majini ambako ndiko kwenye asili ya samaki.

Kwa mujibu wa mtandao wa Venture Tanzania, nguva wanafanana na samaki pomboo (dolphin), akiwa katika kundi la mamalia na sio samaki na wanaishi katika maji ya kina kifupi, katika maeneo yote ya Bahari ya Hindi na Pasifiki.

Wanasema, nguva wanahifadhiwa rasmi chini ya sheria za taifa zinazosimamia uvuvi nchini na wameorodheshwa na Shirikisho la Uhifadhi Duniani (IUCN), kama wanyama walio katika tishio la kutoweka

Kuna wataalamu wanaofafanua kwamba, nguva au kitaalamu 'sirenia' anatambuliwa kuwa mnyama makubwa anayeishi baharini, mwenye uwezo wa kuzaa watoto na wanawanyonyesha maziwa.

Jina la kisayansi 'sirenia' linatokana na neno la Kigiriki na 'nguva' ikiabeba maana "...mwenye mwili wa mwanamke na mkia wa samaki."

Maumbile yake, ana mikono na mkia wenye umbo la pembetatu na urefu kati ya mita mbili na nusu hadi nne na uzito wake unafika tani moja na nusu (kilo 1,500).

Jina alilopewa 'ngombe wa baharini' linatokana na ukweli nguva hula majani ya baharini ambayo hutengeneza nyanda za malisho kwenye maji ya pwani zilizotulia.

Kadri nguva wafanyavyo malisho, hung'oa mmea wote na kuacha alama ya sehemu walizokula, hivyo kwa watafiti inakuwa rahis kuweza kufuatilia malisho na makazi ya nguva kwa kufuata walizokula.

### ANAKOPATIKANA


Kuhusu mahali wanakopatikana jirani nchini, wako kwenye Pwani za Bahari ya Hindi na Karibiani, Pwani ya Afrika ya Magharibi na Mto Amazon.

Mnyama huyo wa baharini ambaye anadaiwa ameanza kutoweka nchini, anaelezwa alikuwa akionekana zaidi katika Pwani ya Dar es Salaam; Kimbiji na Buyuni.

Pia, wataalamu wa elimu bahari wanahimiza umuhimu wa kuwekwa maeneo tengefu ya kuhifadhi wanyama na maisha mapya ya nguva tangu mwaka 1960 wakitawanyika katika delta za Somanga Kilwa mkoani Lindi na Muhoro, Rufuji na Mafia, mkoani Pwani.

Historia ya mnayama nguva, anaelezwa na wataalamu amekuwa akionekana katika zama kabla ya miaka ya 1950 huko Kilwa Kisiwani na Kilwa Masoko mkoa wa Lindi.

> **Historia ya mnyama nguva, anaelezwa na wataalamu amekuwa akionekana katika zama kabla ya miaka ya 1950 huko Kilwa Kisiwani na Kilwa Masoko mkoa wa Lindi na Mwajaa.**



Baadaye katika miaka ya 1980, anaelezwa alionekana Kaole, Bagamoyo na simulizi za kihistoria zikaendelea kuonekana katika maeneo kama Somanga, Kilwa, Lamu (Kenya), Pangani, Buyuni, Kimbiji, Unguja, Pemba, Mafia na Kisiju

### UHAI WAKE

Nguva wanaweza kuishi maisha marefu hadi kufikia miaka 1970. Anaanza kuzaa anapokuwa na umri kati ya 10 na 17 na hiyo, inadumu kati ya miezi 13 hadi 15 na huzaa mtoto mmoja tu.

Mtoto aliyezaliwa anaweza kufikia uzito wa kilo 30 na hunyonya kwa kipindi cha miaka miwili na nusu hadi mitatu. Endapo nguva jike atazaa mtoto dume, huwa anajitenga na nguva wengine kwa kuhofia mtoto wake kuuawa na dume kubwa katika kundi.

Hivyo, kiumbe huyo atabaki mbali na kundi hadi pale mtoto wake atakapokuwa na uwezo wa kujihami na dume kubwa katika kundi. Ndivyo ilivyo.

Inaelezwa kitaalamu, kuadimika kwa nguva, kunaendana na kuwepo simulizi za kupotosha kuhusu kiumbe hicho.

Pindi nguva anaponyonyesha, inaelezwa huwa anakaa katika mtindo wa kusimama, hali inayowafanya baadhi ya watu kumfananisha kiumbe hicho na tafsiri potofu kutoka kwa baadhi ya watu; ikiwaacha swali, nguva ni mnyama au mtu?

Kwa mujibu wa wataalamu, nguva ni mnyama anayezaa kila baada ya miaka mitatu hadi saba watoto hao, akiwa na uzito kati ya kilo 150 hadi 200 na anapofika umri mkubwa, uzito unafika kilo 400 hadi 1,000. Upatikanaji wake unategemea kiasi bahari imechufuka, kwani anapenda kuishi mahali patulivu na akikimbia mambo kama uvuvi haramu unaoathiri viumbe baharini.

Mnyama huyo anayependelea kula majani yaliyo chini ya habari, maarufu kama mwani, umbile lake ni kubwa na lililonyooka na uso wake unafanana na nguruwe, ikiwa rangi ya kijivu na kwa jike ana chuchu kifuani.

Namna anavyoishi katika maji, ana kawaida ya kutoa kichwa juu ya maji, hali inayomuwezesha kuvuta hewa kwa kutumia mashimo mawili ya pua zake kichwani.

Inaelezwa na mamlaka za kiserikali na wadau wa kuhifadhi rasilimali bahari, wavuvi wanapokuwa katika shughuli zao wasimvue.

Katika sura ya pili ni kwamba, kuna wavuvi ambao wameshawavua na kuwala wakieleza nyama yake inakaribia kufanana na ng'ombe.

### MWELEKEO WAKE

Ni mnyama bahari anayeelezwa kuwa na aibu sana na pindi anapogundua kuna binadamu jirani, ana kawaida ya kuhama mbali zaidi,

Wataalamu awanaainisha kwamba, ajali zinazochangia ama vifo au kudhurika kwa nguva, ni matokeo ya ajali za ama bahati mbaya kama kunasa kwenye vyombo vya uvuvi ikiwamo mishipi, jambo ambalo serikali inalazimika kuongeza elimu ya bahari.

Pia, wataalamu wa elimu bahari wanahimiza umuhimu wa kuwekwa maeneo tengefu ya kuhifadhi wanyama na maisha mapya ya nguva tangu mwaka 1960 wakitawanyika katika delta za Somanga Kilwa mkoani Lindi na Muhoro, Rufuji na Mafia, mkoani Pwani.

Historia ya mnyama nguva, anaelezwa na wataalamu amekuwa akionekana katika zama kabla ya miaka ya 1950 huko Kilwa Kisiwani na Kilwa Masoko mkoa wa Lindi na Mwajaa.

Baada ya miongo kadhaa akadaiwa alionekana huko Kaole, Bagamoyo na simulizi za kihistoria zinangusa, Somanga, Kilwa, Pangani, Buyuni, Kimbiji, Kisiju, Unguja, Pemba, Mafia na Lamu Kenya.

***Makala hii ni kwa mujibu wa mijadala, taarifa na maandiko mbalimbali ya kitaaluma.***



# Kanisa Anglikana lasitisha maadhimisho ya miaka 50

**Na Peter Mkwavila**
DODOMA

KANISA Anglikana Tanzania, limesitisha maadhimisho ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwake nchini ili kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Hatua hiyo ilitangazwa na Msaidizi wa Mkuu wa Kanisa hilo nchini, Dk. Dickson Chilongani, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma.

Dk. Chilongani alisema kuwa wamechukua hatua hiyo ili kuitikia wito wa serikali wa kuepukana na mikusanyiko yote.

Dk. Chilongani ambaye pia ni Askofu wa Kanisa hilo Dayosisi ya Kati, alisema kuwa sherehe zilitakiwa kufanyika Septemba mwaka huu makao makuu ya Dodoma na kuhudhuriwa na maaskofu,wachungaji na waumini kutoka kwenye dayosisi zilitarajiwa.

Alisema kwenye maadhimisho hayo mambo muhimu ambayo yalitakiwa kufanyika ni upandaji miti zaidi ya milioni 10 karibu mikoa yote ya nchi.

Alisema Kanisa la Angalikana Tanzania likiongozwa na mkuu wa kanisa wamechukua hatua hiyo ya kuahirisha kwa ajili ya kuzuia maambukizi hadi mwakani hali ikiwa mzuri.

Aidha, alisema hatua hiyo ya kuhahirisha sherehe hiyo ni pamoja na kutii agizo la serikali katika kuzuia mikusanyiko.

“Sherehe hiyo ilitakiwa ifanyike hapa na tungekusanyika wachungaji wote kutoka dayosisi za nchi mzima hapa UDOM na tuwe na ibada maalum ambayo tungeifanya hapa uwanja wa mpira wa Dodoma kwa ajili ya shamrashamra ya kusherehekea miaka hiyo 50,” alisema.



Mjasiriamali ambaye jina lake halikupatikana, akitafuta wateja kama alivyokutwa barabara ya CDA jijini Dodoma. Biashara ndogo zimetoa msaada wa ajira kwa makundi ya watu wengi nchini. **PICHA:.IBRAHIM JOSEPH**

# Diwani apiga marufuku uingizaji taka vifungashio

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

DIWANI wa Kata ya Chamwino jijini Dodoma, Jumanne Ngede, amepiga marufuku uingizwaji wa taka za vifungashio vinavyoletwa na bidhaa mbalimbali kwenye dampo la soko la Bonanza zinazozalishwa na wafanyabiashara kutoka nje.

Vifungashio hivyo vilivyozuiliwa kwenye dampo hilo la soko ni vile vinavyoletwa huku vikiwa vimefungashwa kwenye matunda ikiwamo ndizi, miwa, nyanya, machungwa na mahindi mabichi.

Ngede, alipiga marufuku hiyo wakati alipokuwa akizungumza na viongozi wa soko hilo la Bonanza jijini Dodoma, kwenye kikao cha kujadili uondoshwaji wa taka hizo zinazoletwa na wafanyabiashara wa kutoka nje.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya halmashauri ya jiji, wale wote watakaobainika kutupa taka hizo kwenye dampo sokoni, faini inayotozwa ni kuanzia kiasi cha Sh. 50,000 hadi 300,000.

Alisema faini hizo zimewekwa kwa wale watakaobainika kukiuka katazo hilo la kuzitupa taka hizo kwenye dampo hilo ikiwamo makosa mengineyo kwa mujibu wa kanuni na sheria.

Hata hivyo alisema kuwa, kwa wafanyabiashara hao wanatakiwa wanapoleta bidhaa zao kuondokanazo na kupeleka kwenye dampo lililotegwa eneo la Chidaya ambalo lipo kwa ajili ya kuhifadhi taka ambalo ni la kisasa.

“Lengo la jiji ni kuona mji wake unakuwa katika mazingira safi na hauelemewi na wingi wa taka zozote za kutoka nje kwa kuwa wao hawahusiki, hivyo ninawaagiza nyinyi viongozi wa soko hili la Bonanza wafanyabiashara hao wanaoleta bidhaa kuzingatia sheria na kanuni na wanaokiuka wachukulieni sheria kali ikiwa na kulipa faini,” alisema.

Diwani huyo pia aliwataka wafanyabiashara na viongozi kuunda kikosi ambacho kitahakikisha dampo hilo halitumiki kwa kutupa taka za vifungashio na pindi wanapoona taka hizo zikitupwa kwenye eneo hilo wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Kwa upande wake Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alisema kuwa Halmashauri ya Jiji imeshatoa maelekezo ya kuwataka wafanyabiashara wote wanaoleta bidhaa zao zikiwa kwenye vifungashio wanaondokanazo.

Aidha, alisema ili waweze kudhibiti hali hiyo wafanyabiashara wenyewe wanatakiwa kutoa ushirikiana na halmashauri ya jiji ili kudhibiti hali hiyo ndani ya masoko yote ambayo tayari yameshapewa maelekezo ya kutotupa vifungashio hivyo.

Pia aliwataka wafanyabiashara ndani ya masoko yote ya jiji kuhakikisha wanazingatia usafi wa mazingira wanayofanyia kazi badala ya kusubiri kufanyiwa na watu wengine.

Alisema hatua hiyo pia lengo ni kuepukana na kufanyabishara kwenye maeneo yasiyo rafiki kwao na wateja wanaowahudumia.

# Wakulima mtama wakumbukwa bima

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

WAKULIMA wa mtama wilayani Kongwa, mkoani Dodoma, wamekatiwa bima ya zao hilo na kampuni ya vinywaji ya Tanzania Breweries Ltd (TBL).

Wakizungumza na waandishi wa habari wilayani hapa, wakulima hao walisema kuwa wamefurahishwa na hatua hiyo ya kukatiwa bima ya zao hilo na kampuni hiyo.

Mmoja wa wakulima hao kutoka Kijiji cha Sagala ‘B’, wilayani hapa, Hilda Madeje, alisema wamefurahia kilimo hicho mwaka huu kutokana na kukatiwa bima ya zao hilo na kampuni ya Tbl.

“Tumekuwa tukilima zao hilo miaka mingi, lakini kwa mwaka huu TBL wametusaidia kwa kutuakatia bima ya mazao hayo, hivyo hakuna atakayepata hasara kwa msimu huu,” alisema.

Madeje alisema bima hiyo itawafidia wakulima ambao mazao yao yataathiriwa na majanga kama mvua, upepo mkali na shamba kuharibiwa na wadudu waharibifu wa mazao.

Alisema uwapo wa bima hiyo utamfidia mkulima ambaye amejiunga kundi la kilimo cha mtama, ambao unahitajika na Tbl kwa ajili ya kuzalisha mmoja ya kinywaji kinachozalishwa kwenye viwanda vyake.

Naye Mariam Magala, alisema kilimo cha zao hilo kimewanufaisha baadhi ya wakulima kutokana na kupewa mbegu na kuwa wanufaika wa soko baada ya kuvuna.

Magala alitaja faida nyingine ya zao la mtama kuwa ni kuwa na uhakika wa chakula cha familia kutokana na aina hiyo.

Kwa upande wake Meneja wa kilimo wa TBL, Joel Msechu, alisema wameanza kwa wakulima wachache ili wengine watakapoona mafanikio ya wenzao watavutiwa na kujiunga kulima zao hilo.

Msechu alisema wameweka mawakala wa kusambaza mbegu bora kila mikoa ili kuwasaidia wakulima pamoja na kuwakatia bima ili kuwafidia watakaokumbwa na majanga mbalimbali.

“Ndugu yangu, kilimo kina changamoto mbalimbali, tumeona kuwasaidia wakulima wetu ili kuepuka hasara zikiwapata baadhi yao na kujutia kazi hito,” alisema.

Alibainisha kuwa mategemeo yao ni kuhakikisha kila mkulima aliyeingia mktaba na kampuni hiyo ananufaika katika kilimo hicho ili kuinua uchumi wa familia za wakulima.





## Soko la ndizi laporomoka kisa corona

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SOKO la ndizi katika wilaya ya Rungwe, limeanza kuporomoka kutokana na wanunuzi wa ndani na nje ya nchi kupungua kwa sababu ya tishio la ugonjwa wa corona ambao unasambaa kwa kasi duniani.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ezekiel Mwankota, alisema ndizi za Wilaya hiyo zimekuwa zikiuzwa katika nchi za Zambia na Malawi ambazo kwa sasa zimefunga mipaka yao ili kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema kutokana na hali hiyo, ndizi zimeanza kukosa soko la nje na limebakia soko la ndani ambalo halina faida kwa wakulima kama lilivyo la nje ambalo limekuwa likiwasaidia wakulima kunufaika na kilimo chao. "Kwa sasa tumeanza tunauziana sisi kwa sisi ndani ya nchi, hakuna wateja wale wa kutoka nchi jirani za Zambia na Malawi ambazo ndizo zilikuwa zinanunua kwa wingi, sasa tunaona athari za ugonjwa huu zimeanza kutukumba," alisema Mwankota.

Aliwataka wananchi wa wilaya hiyo pamoja na wageni wote kuendelea kuchukua tahadhari zinazoelekezwa na wataalamu ili ugonjwa huo usiendelee kusambaa na kuathiri sekta mbalimbali nchini.

Baadhi ya wakulima wilayani humo walisema soko la ndizi lilikuwa limeimarika baada ya Serikali kupiga marufuku tabia ya baadhi ya wafanyabiashara kuchimbia ndizi zikiwa bado hazijakomaa mashambani.

Mmoja wa wakulima hao, Sekela Mwakitalu, alisema biashara ya kuchimbia ndizi ilikoma baada ya Serikali kutoa elimu kwa wakulima pamoja na kufungua masoko maalumu ya kuuzia zao hilo ambapo wateja wananunua kupitia mifumo rasmi. Alisema kabla ya ugonjwa wa corona kuingia nchini walikuwa wanauza mpaka Sh. 15,000 kwa mkungu mmoja, lakini sasa hivi zimeshuka tena na kufikia mpaka Sh. 5,000, hali ambayo alidai inatishia kilimo cha zao hilo.

"Tulikuwa tumefikia kipindi ambacho tulikuwa tunafaidi kilimo chetu, tulipoachana na wale wachumbiaji tulikuwa tunalima na kuvuna ndizi zetu kwa muda ambao tunataka sisi wenyewe na tulikuwa tunauza kwa bei nzuri lakini sasa hali imekuwa mbaya," alisema Mwakitalu.

Naye Osward Kasanga, alisema endapo ugonjwa huo utaendelea kusambaa kuna uwezekano soko la ndizi likafa kabisa, hivyo wakulima kupata hasara kubwa.

Alisema kutokana na kudorora kwa soko la ndizi hizo, baadhi zimeanza kuiva zikiwa sokoni kutokana na kuhifadhiwa muda mrefu bila kununuliwa.

# DC afanya ziara za kushtukiza kwenye taasisi, kampuni corona

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Maryprisca Mahundi, ameanza kufanya ziara za kushtukiza kwenye kampuni na taasisi mbalimbali wilayani humo kukagua utekelezaji wa maelekezo ya Serikali kwa waajiri kuwakinga wafanyakazi wao dhidi ya ugonjwa wa corona.

Mahundi alianza ziara hizo juzi akiwa ameambatana na Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Felister Kisandu na Ofisa Afya wa Wilaya hiyo, Mgonga Melick, walifanya ukaguzi wa kushtukiza katika kambi ya kampuni ya mkandarasi anayejenga barabara ya Chunya-Makongolosi yenye urefu wa kilomita 39 iliyopo katika Kata ya Matundasi.

Alisema moja kati ya vitu ambavyo walikuwa wanakagua ni kuangalia endapo viongozi wa kampuni wanawapatia wafanyakazi wao barakoa kila asubuhi wanapoanza kazi pamoja na kuandaa maji yanayotiririka na sabuni kwa ajili ya kunawa.

Alisema vilevile, walikuwa wanakagua kama kampuni hiyo pamoja na taasisi zingine kama zinaandaa vitakasa mikono kwa ajili ya wafanyakazi wao ili kuwakinga dhidi ya virusi vya corona ambavyo vimekuwa tishio duniani kote.

"Nimefurahishwa na namna ambavyo kampuni hii inatekeleza maelekezo, hawa wameenda mbali zaidi kwa kuandaa mpaka chumba maalumu cha kuwatenga watu watakaoshukiwa kuwa na ugonjwa huu kabla hawajapelekwa kwenye vituo vilivyoandaliwa na Serikali," alisema Mahundi

Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Kisandu, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa kada zote ili kuhakikisha wanaepuka ugonjwa huo.

Alisema moja kati ya mambo ambayo wanawazuia ni kufanya mikusanyiko ya aina yoyote na kwamba hata ikitokea msiba wakishazika wanatakiwa kutawanyika kila mtu kurudi nyumbani.

Alisema pia wanawasisitiza kuacha tabia ya kusalimiana kwa mikono na kukumbatiana kwa maelezo kuwa vitendo hivyo ndivyo vinavyopelekea watu kuwa katika hatari zaidi ya kuambukizwa ugonjwa huo.

"Tunataka wananchi wawe katika tahadhari ya hali ya juu, sasa inatakiwa kampuni zote na taasisi zote zenye mkusanyiko wa watu wengi kuweka mazingira ya tahadhari kama walivyofanya hawa wachina," alisema Dk. Kisandu.

Meneja wa Kampuni hiyo, Song Gao, alisema wametii agizo la serikali kutokana na hatari ya ugonjwa huo hasa ikizingatiwa wao wana watumishi wengi hivyo ni lazima waungane na serikali katika mapambano hayo.

Alisema kampuni hiyo ina zaidi ya wafanyakazi 100 ambao wamegawanyika katika makundi mbalimbali na kwamba kutokana na idadi hiyo ya wafanyakazi kunakuwa na hatari kubwa ya kuambukizana ugonjwa huo endapo mmoja wao atakuwa nao.

"Kila asubuhi tunapoanza kazi tunagawa barakoa kwa wafanyakazi wetu wote, lakini kila sehemu tumeweka maji yanayotiririka na sabuni kwa ajili ya wafanyakazi na wageni wetu kunawa mikono," alisema Gao.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa wilaya hiyo, aliwataka Askari wa usalama barabarani kuhakikisha magari ya abiria yanakuwa na vitakasa mikono kwa ajili ya abiria na hayajazi abiria kupita kiasi yanapoingia au kutoka katika wilaya hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Maryprisca Mahundi (wa pili kushoto), akizungumza na viongozi wa kampuni ya kichina inayojenga barabara ya Chunya - Makongolosi kwa kiwango cha lami, kuhusu utaratibu wa kuwakinga wafanyakazi wao dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa Corona. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Sababu TFS kuongeza uzalishaji miti

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imeamua kuzalisha miche kati 800,000 hadi 1,000,000 kila mwaka kwa lengo la kukabiliana na vitendo vya uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji miti katika jamii.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja Msaidizi Usimamizi Rasilimali wa FSF, Innocent Lupembe wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakati akizungumzia jitihada zinazofanywa na ofisi hiyo katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira ndani ya jamii.

Alisema TFS imekuwa ikizalisha miche ya aina mbalimbali ikiwamo ya kuni, mbao, matunda, maua na miche ya kivuli, ambayo hugawanywa kwa watu na taasisi mbalimbali katika jamii ili kutunza mazingira.

Alisema ofisi hiyo imekuwa na utamaduni wa kugawa miche hiyo bure kwa watu na taasisi mbalimbali zinazoomba kupata miche hiyo kwa lengo la kwenda kuipanda katika maeneo yaliyoathirika kutokana na vitendo vya ukataji miti hovyo vinavyofanywa na baadhi ya watu.

Lupembe alisema kati ya miche hiyo inayozalishwa, kuna miche ya asili ambayo huzalishwa katika ofisi za TFS, lengo ni kuhakikisha kuna kuwa upandaji wa miche hiyo kwa wingi ili kurudisha uoto wa asili katika maeneo ya misitu ya asili na katika vyanzo vya maji.

"Uzalishaji wa miche hii ya asili umekuwa na umhimu mkubwa katika kukabiliana na uharibifu unaofanywa kwenye maeneo yenye misitu ya asili na katika maeneo ya vyanzo vya maji kwenye maeneo mbalimbali ya mikoa ya kanda ya nyanda za juu kusini," alisema.

Alisema kulingana na takwimu zilizofanywa, zinaonyesha kuwa takribani hekta 372,000 huharibiwa kila mwaka kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu zikiwamo za uchomaji moto ukataji miti kwajili ya kuni.

Pia, alisema ili kuhakikisha kunakuwa na utunzanji bora wa misitu, ofisi hizo za TFS zimekuwa na mpango endelevu wa kugawa mizinga ya nyuki kwa wananchi wanaoishi karibu na misitu iliyohifadhiwa ili waweze kujiongezea kipato badala ya kukata miti kwajili ya mkaa ambao huuzwa.

Alisema hali ya upandaji wa miche ya miti, kugawa mizinga ya nyuki na kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na uhifadhi wa misitu katika mikoa ya nyanda za juu kusini kumechangia kuleta matokeo chanya katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira hapa nchini.







Barabara ya Kivule Makonde, ikiwa imeharibika na kusababisha kero ya kukosekana kwa usafiri wa daladala kwa wananchi wanaotumia barabara hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SMZ yasitisha mikusanyiko Ramadhani/Eid

**Na Hawa Abdallh,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar, imetangaza rasmi kusitisha shughuli zote za kuftarishana, darasa za pamoja za mwezi wa Ramadhan, shughuli za Baraza la Eid pamoja na zinazoambatana na mikusanyiko katika sherehe za Eid.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohammed Aboud Mohammed, wakati akitoa taarifa maalumu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia televisheni ya Taifa ya Zanzibar (ZBC).

Alisema katika kuendelea kuchukua hatua ya kujikinga na kuzidi kuenea kwa virusi vya Corona, serikali inaendelea kusisitiza marufuku ya mikusanyiko katika sherehe zote zinazoambatana na Eid katika kipindi hiki ambacho janga hilo limeikumba dunia.

Pia, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewataka wazazi/walezi kutowaruhusu watoto wao kutoka kwa ajili ya shughuli zozote za sherehe ambazo husababisha mikusanyiko na kushauri watu kubaki nyumbani isipokuwa kwa dharura maalumu.

Aliitaka jamii kuendelea kufuata maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Afya kuhusu ugomjwa wa Covid -19 ikiwamo kujiepusha na mikusanyiko isiyo ya lazima.

Katika Visiwa vya Zanzibar, imezoeleka katika kipindi cha mwezi wa Ramadhani kuwapo na darasa katika misikiti mbalimbali pamoja na sherehe za Eid ambazo husherekewa kwa muda wa siku nne katika maeneo maalumu ambayo serikali inayatenga kwa watoto kufurahi.

# Abiria wapimwa joto la mwili kuepusha maambukizi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mkoa Kusini Unguja, imeanza rasmi kuwapima joto la mwili abiria wa magari yanayotoka mjini kuelekea maeneo mbalimbali ya mkoa huo ili kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya virusi vya Corona.

Upimaji huo umefanyika chini ya Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Mohd Mahmoud, eneo la Jumbi, Wilaya ya Kati kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ili kuweka vizuizi katika mipaka yote ya kuingilia barabara kuu kwa kuwalenga wananchi wanaoingia katika mkoa huo kupimwa.

Alisema hatua hiyo ni moja ya mikakati ya kudhibiti kuenea virusi hivyo pamoja na kuwagundua watu wenye viashiria vya ugonjwa huo kwa kuwapima joto la mwili wasafiri wote na watakaobainika katika zoezi hilo watapelekwa katika kituo cha afya kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Alisema janga hilo ni la duniani hivyo jitihada za kupambana kuhakikisha virusi hivyo havienei kwa kasi na kuleta athari zaidi zinahitajika.

"Jamii inatakiwa kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuzingatia ushauri wote unaotolewa na serikali kupitia Wizara Afya katika kuhakikisha tunajikinga na virusi hivi ambayo vinaenea kwa kasi na kwa mara moja, ni vyema tukazingatia yote tunayoambiwa na wataalam wetu wa afya," alisema.

Vile vile, alisema serikali ya Mkoa wa Kusini Unguja imewasisitiza madereva na makonda wa daladala kufuata sheria na taratibu zinazotolewa na wizara hiyo kutumia njia sahihi za kuwakinga wananchi na ugonjwa huo kwa kuwa wananchi wanategemea zaidi usafiri huo. Katika hatua hiyo Jeshi la Polisi limegundua udanganyifu unaofanywa na baadhi ya madereva kutumia losheni na sabuni kwa kuwapaka abiria badala ya kutumia vitakasa mikono 'sanitizer' kama agizo linavyoelekeza na jumla ya zaidi kesi 18 za madereva na makonda zimefikishwa katika mahakama ya halmashauri ya Wilaya ya Kati na kutozwa faini kwa makosa hayo.

Madereva na wananchi waliofanyiwa vipimo hivyo wameipongeza serikali ya mkoa huo kwa uamuzi huo ambao utasaidia kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huo na kuwaondolea hofu wananchi.

# KIST yakabidhi kifaa cha kitaalamu kunawia mikono

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrisa Muslim Hija, ameishukuru Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume (KIST), kuwapatia kifaa cha kunawia mikono cha kitaalamu ambacho kitasaidia kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona.

Akizungumza wakati wa kukabidhiwa kifaa hicho huko, Wizara ya Elimu Mazizini, Dk. Idrisa alisema kifaa hicho kimeletwa muda muafaka.

Alisema ubunifu huo wa kutengenezwa kifaa hicho ndio unaotarajiwa na wizara katika kipindi hiki, ambacho mbali na ujuzi wanaoandaliwa, pia wanakuwa na ubunifu kutokana na mahitaji yanapojitokeza katika jamii hasa kwa sasa.

"Wasomi wanatakiwa kubuni mambo ambayo yanaendana na mahitaji ya jamii kwa wakati sahihi, kama ilivyo hivi sasa suala la kunawa maji mikono linahitajika zaidi japo bado njia inayotumika katika unawaji pia sio salama kwa asilimia zote kwakuwa kila mtu anakamata bomba la kunawia," alisema.

Pia, aliupongeza uongozi wa KIST kwa juhudi wanazozichukua kuendeleza elimu kwa vijana na kuwashukuru kuipatia wizara yao kifaa hicho.

Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume KIST, Dk. Bakari Ali Silima akikabidhi kifaa hicho alisema chuo hicho kimekuwa kinatimiza malengo yake ya kubuni vitu ambavyo vinaweza kusaidia jamii mbali na teknolojia kubwa.

Alisema kifaa hicho kitasaidia usalama zaidi wa kiafya kwa kupunguza kukamata kifuniko cha sabuni kwa kutumia mikono kama ilivyozoeleka badala yake inatumika miguu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**Getruda Mtani Mganga** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato nne chenye index namba **S0849-0018** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika SHule ya Sekondari Morembe . Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MUS/RB/8964/2018**

115711502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Ndugu, STEPHEN PASCHAL MAKINGO** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari Yenye namba za usajili **T 809 DHN.** Kwa yeyote atakae iona Atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu kwa Kumb: **MWA/NY/RB/319985/2020.**

215712202

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MAKERA INVESTMENT COMPANY LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA **SANLG** YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 345 BZF.** KWAYOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **KAH/ / RB/ 145/2020**

115712302

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**'WAMILIKI WA KAMPUNI YA WESHARE MICROFINANCE COMPANY LIMITED** (NAMBA YA USAJILI 141173499 YA TAREHE 03/03/2020) ,WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA WAMEKUKUBALIANA KWA HIYARI YAO KUFUNGA KAMPUNI'

115711602

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Rotary zasaidia Ilala, Temeke

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU za Rotary za Bahari na Dar es Salaam, zimetoa msaada wa barakoa zikiwamo za watoa huduma pamoja na gloves za kufanyia uchunguzi zenye thamani ya Sh. milioni 17 kwa hospitali za rufani za Ilala na Temeke.

Msaada huo ni sehemu klabu za rotary kusaidia kuwakinga madaktari na manesi, ambao wapo mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya corona.

Akizungumza katika makabidhiano, Rais wa Rotary Club ya Bahari, Hitesh Tanna, alisema msaada huo pia utawasaidia wanataaluma ya tiba kutekeleza majukumu yao katika mazingira salama, na kuepukana na tahari ya kuambukizwa.

"Rotary ni sehemu ya jamii, na tunaamini kuwa ni muhimu kufanya tutakaloweza kuiunga mkono serikali katika kipindi hiki," alisema.

Aidha, alisema kuwa klabu za Rotary zinajipanga kutafuta zaidi wa Sh. milioni 200 kwa ajili ya kusaidia vifaa zaidi.

Tanna aliwataka watu wengine wenye nia njema kuendelea kuisaidia serikali katika mapambano dhidi ya Covid-19.

## MNH yasambaza mavazi maalum

**Na Enock Charles**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili, imeanza kusambaza mavazi maalumu (coverall) ambayo ni sehemu ya mavazi ya watoa huduma (PPE) kuvaa ili kujikinga wakati wanatoa huduma kwa wagonjwa wenye maambuki mbalimbali ikiwamo Covid 19 kwa kamati za dharura za jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na wanahabari , Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Zuhura Mawona, alisema kuwa baada ya kujadiliana na Serikali bei elekezi itakuwa Sh. 50,000 kwa vazi moja.

Manispaa ya Kinondoni imenunua mavazi 15 yenye thamani ya Sh. 750,000, Ilala mavazi 20 yenye thamani yaSh.. 1,000,000, huku Manispaa nyingine zikiendelea kulipia ili kupata mavazi hayo.

"Kwa sasa tunaanza na vituo vilivyopo katika Manispaa za Jiji la Dar es Salaam na mikoa mingine itafuata" alisema Mawona

Alisema mahitaji ni makubwa katika mikoa mbalimbali hivyo kwa sasa Muhimbili imejikita katika kuongeza uzalishaji ili kukidhi mahitaji.

Wiki iliyopita Muhimbili ilizindua vazi hilo maalumu liloshonwa na wataalamu wa MNH kwa kutumia malighafi za ndani ya nchi lengo i kukabiliana na upungufu wa bidhaa hizo.

# Kigogo kontena aamriwa kulipa fidia ya mil. 207/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imemhukumu Mkurugenzi wa Kampuni ya Salsabil Investment Ltd, Abdulrahman Omary (55), kulipa fidia ya Sh. milioni 207, baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kukutwa na kontena 17 za mazao ya misitu aina ya magogo zenye thamani ya Sh. milioni 452 bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Maliasili.

Kadhalika, mahakama hiyo imemhukumu kulipa faini ya Sh. milioni moja au kwenda jela miaka miwili baada ya kukiri kosa la kukutwa na kontena hizo bila kibali ikiwamo kutaifishwa kontena hizo zilizopo Bandari Kavu Ubungo Maziwa, jijini Dar es Salaam.

Hukumu hiyo ilisomwa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya mshtakiwa kuingia makubaliano na Mkurugenzi wa Mashitaka Nchini (DPP) ya kulipa kiasi hicho cha fedha na kwamba tayari alifanikiwa kulipa na kukabidhi risiti hiyo mahakamani.

Awali, mshtakiwa alikuwa anakabiliwa na mashtaka 15 ya uhujumu uchumi ikiwamo kukutwa na mazao ya misitu na kutakatisha fedha, lakini aliingia makubaliano na DPP ya kukiri tuhuma zinazomkabili.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladslaus Komanya, akisaidiana na Wakili wa Serikali Mkuu, Materus Marandu, aliomba mahakama imfutie mshtakiwa shtaka la uhujumu uchumi na baada ya maombi hayo alitoa hati mpya ya mashtaka kutoka kwa DPP ya kuipa mamlaka mahakama hiyo kusikiliza kesi hiyo.

Komanya alidai DPP aliamua kuyaondoa mashtaka 14 hivyo kuomba kumsomea upya hati ya mashtaka ambayo ni kukutwa na magogo hayo bila kuwa na kibali.

Inadaiwa mshtakiwa kati ya Januari Mosi 2015 na Novemba 31, mwaka 2015, katika maeneo tofauti Ex Nasaco wilayani Ilala, Dar es Salaam, alikutwa na mazao ya misitu ya African Rose Wood, yenye thamani ya Sh. 452, 787, 076, bila kuwa na kibali.




Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Angelina Ngalula (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, alipokuwa akitambulisha kamati ya ushauri yenye wajumbe 14 kwa lengo la kutoa tathmini na ushauri kuhusu athari za kiuchumi zinazotokana na maambukizi ya ugonjwa wa corona katika kongani zote za sekta binafsi. Kushoto ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara, Dk. Godwill Wanga. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Waziri: Uzalishaji korosho umefika tani milioni moja

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga (pichani), ametoa taarifa ya uzalishaji wa zao la korosho katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, akibainisha kuwa umefikia tani 1,036,698.

Amesema kiasi hicho kimeiingiza nchi Sh. trilioni 3.3 na fedha za kigeni Dola bilioni 1.139 kwa kipindi cha miaka mitatu (2017-2019), hivyo zao hilo kuongoza kwa mauzo kuliko mazao yote nchini.

Katika kutekeleza sera ya viwanda ya serikali, Waziri Hasunga alisema jana kuwa, viwanda vya kubangua korosho vimeongezeka kufikia 30 kutoka 21.

Katika taarifa hiyo, waziri huyo pia alisema uzalishaji wa korosho nchini umeongezeka kwa kuwa mpaka sasa, jumla ya mikoa 20 inazalisha korosho kulinganisha na mikoa mitano pekee kabla ya serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani.



"Watanzania wengi wamehamasika na kilimo hicho ambapo mikoa hiyo imeamua kujishughulisha na zao hilo kutokana na umuhimu wake katika mapato ya wakulima na Watanzania kwa ujumla wake," alisema.

Kwa mujibu wa waziri huyo, takribani Watanzania milioni 1.6 wameajiriwa katika zao hilo, jambo ambalo limewanufaisha na kujipatia kipato.

Alisema mafanikio hayo yametokana na namna ambavyo serikali imetoa elimu kwa kina kuhusu namna bora ya kutumia viuatilifu, kuongeza uzalishaji na tija, kadhalika uwekezaji katika eneo la utafiti kupitia Kituo cha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo cha Korosho cha Naliendele kilichoko Mkoani Mtwara.

Alisema kituo hicho kimefanya kazi kubwa na nzuri ya kuhakikisha kuwa wakulima wanapata miche bora ya mikorosho, yenye uwezo wa kuongeza uzalishaji, zenye uwezo wa kustahimili ukame, na zenye uwezo wa kukinzana na magonjwa mbalimbali, hivyo kuwa kitovu cha uzalishaji wa miche ya mikorosho nchini.

Waziri Hasunga alisema katika kipindi hicho ubora wa korosho umeimarika hivyo kupelekea korosho ya Tanzania kupendwa na kuvutia wanunuzi wengi duniani.

## HABARI MICHEZO

# MAGUIRE AFUNGUKA WANACHO KITAFUTA UNITED



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United, haina furaha kuwa kwenye nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kwa sababu wanataka kushinda mataji, na Harry Maguire anahisi bado hawapo kwenye njia sahihi kufanikisha hilo.

Baada ya kutawala Ligi Kuu England chini ya Alex Ferguson, United imeshindwa kuwa kileleni katika msimamo wa ligi hiyo tangu alipoondoka kocha huyo mwaka 2013.

Louis van Gaal aliwaongoza mashetani wekundu hao kutwaa taji la FA mwaka 2016 na Jose Mourinho akatwaa Kombe la Ligi na Ligi ya Europa miaka miwili iliyofuata.

United ipo nafasi ya tano kwenye msimamo, ikipitwa pointi tatu na Chelsea waliopo nafasi ya nne, wakati ligi hiyo ikisimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona Machi, mwaka huu.

Maguire, ambaye aliwasili kutoka Leicester City kwa ada ya pauni milioni 80 Agosti mwaka jana, anaamini Ole Gunnar Solskjaer ana timu ambayo itamwezesha kurudisha umwamba wake kwenye soka la Uingereza.

"Nafikiri unaweza kuona tangu mwanzo mwa msimu, tunaonekana kama timu. Unaweza kuona wapi tunakwenda, wapi tulipokuwa," amesema Maguire akiiambia Sky Sports.

# Liverpool ndio timu iliyokamilika EPL – Lovren

**LIVERPOOL,** England

DEJAN Lovren anaamini Liverpool bado wanaweza kuwa bora zaidi wakati akizungumzia kikosi kilichokamilika zaidi kwenye Ligi Kuu England.

Vijana hao wa Jurgen Klopp walikuwa wanaongoza kwa tofauti ya pointi 25 kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England wakati msimu uliposimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Wakiwa wametoka kupata mafanikio ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, Liverpool wapo kwenye nafasi nzuri ya kushinda taji jingine msimu huu.

Lovren mwenye umri wa miaka 30, bado anaamini kikosi hicho cha Klopp kinaweza kuimarika, huku akisifia uwiano uliopo ndani ya timu hiyo.

"Ni muhimu kuwa na kikosi kilicho na mchanganyiko na wachezaji vijana, umri wa kati na wachezaji wenye uzoefu.

"Nafikiri sisi tuna vitu vyote hivyo, ni timu yenye uwiano mzuri," amesema beki huyo wa kimataifa wa Croatia akinukuliwa na tovuti yake.

"Tumezoea kucheza kwenye fainali kubwa na timu kubwa na tunajua namna gani ya kujipanga.





# *Balotelli: Binti yangu ananifanya niifikirie Napoli*

**NAPLES,** Italia

MARIO Balotelli amesisitiza bado ana nia ya kuichezea Napoli kwa sababu ndiyo timu inayoshabikiwa na binti yake.

Balotelli alijiunga na timu ya nyumbani kwake, Brescia Agosti mwaka jana, lakini alihusishwa na kutua pale Napoli.

Mchezaji huyo wa zamani wa AC Milan, Inter na Liverpool amesema alijaribu kujiunga na Napoli na akabainisha bado angependa kuhamia pale kwenye Uwanja wa San Paolo.

"Nitakuwa na wakati mzuri nikiwa pale mji wa Naples. Binti yangu atafurahia sana, kwa sababu ni shabiki wa Napoli.

"Namwimbia, 'Brescia, Brescia', lakini yeye anaipenda zaidi Napoli. Alifurahi sana nilipompeleka kwenye Uwanja wa San Paolo.

"Mara zote kunahisia nzuri kuingia kwenye Uwanja wa San Paolo, ingawa kwa maoni yangu uwanja mzuri zaidi ni San Siro."

Balotelli amefunga mabao matano katika mechi 19 za Serie A msimu huu kabla ya ligi kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Balotelli mwenye umri wa miaka 29, ameichezea Timu ya Taifa ya Italia mechi 36 na kwa mara ya mwisho alicheza mwaka 2018 na amesema anataka kurudi tena na kumheshimu kocha, Roberto Mancini.

# Barcelona kuuza haki ya jina la Camp Nou

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona inadhamiria kuuza haki za jina la Uwanja wa Camp Nou, msimu ujao ikiwa ni sehemu ya kutafuta fedha kwa ajili ya kupambana na mlipuko wa corona.

Katika taarifa yake Jumanne, Barca ilisema haki za uwanja huo zitaongeza kwenye mfuko wa klabu baada ya kuuza jina hilo kwa mdhamini.


Fedha zitakazopatikana kwa msimu wa 2020-21 zitatumika kwenye miradi ya Katalunya na sehemu nyingine duniani kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa homa ya mapafu maarufu kama COVID-19.

Barca hapo awali haijawahi kutoa ofa ya kuuza haki ya jina la uwanja wake.

"Ni wakati muhimu kwa duniani, kwa afya, uchumi na janga la kijamii kwenye historia ya duniani," ilisema taarifa ya Barca.

"FC Barcelona imechukua maamuzi ya aina yake, kwa ajili ya kutoa jibu la janga la kibinadamu ambako kila mmoja anatakiwa kuwajibika kwa nafasi yake.

Majadiliano zaidi yatachukuliwa wiki ijayo ili kutafuta mdhamnini ambaye atakuwa tayari kununua haki za uwanja huo.







# JORGINHO KUONGEZA MKATABA CHELSEA

**LONDON,** England

WAKALA wa Jorginho amebainisha kwamba kiungo huyo anaweza kuongeza mkataba mwingine wa kuendelea kuitumikia Chelsea wakati akikanusha uvumi wa kutakiwa na Juventus.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua Turin, sehemu ambayo yuko kocha wake wa zamani aliyemnoa Napoli na Chelsea, Maurizio Sarri.

Hata hivyo, wakala wa Jorginho, Joao Santos – amesisitiza hajasikia lolote kutoka Juventus kumhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.

Na Santos amesema Jorginho anaweza kuongeza mkataba wake na klabu hiyo ya Ligi Kuu England, ambapo mkataba wake wa sasa unamalizika ifikapo mwaka 2023.

"Juventus? Nilisoma sehemu, lakini sijawahi kuwasiliana nao," alisema akiiambia CalcioMercato.

"Hadi sasa, kwa kweli sijui chochote kuhusu hali ilivyo.

"Yeye ana furaha kubwa kuwa katika jiji la London, ambako amekuwa akionyesha thamani yake na sehemu ambayo bado ana miaka mingi kwenye mkataba wake.

"Na Julai, kuna uwezekano akaongeza mwaka mmoja kwenye makubaliano yao na kufungua milango ya majadiliano mapya na Chelsea."

Jorginho amecheza mechi 26 kwenye Ligi Kuu England, akifunga mabao manne msimu huu kabla ya msimu kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

# Ligi Kuu Uholanzi kutoendelea tena

**AMSTERDAM,** Uholanzi

MSIMU wa Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, ni kama hautaendelea tena baada ya Shirikisho la Soka la Uholanzi (KNVB), kutangaza "halina mpango wa kuendelea" na msimu wa 2019-20 baada ya serikali kuongeza siku za watu kukaa ndani na kutoruhusu mikusanyiko.

Jumanne wiki hii, Waziri Mkuu wa Uholanzi, Mark Rutte, aliongeza muda wa kutotoka nje hadi Septemba Mosi, mwaka huu wakati wakiendelea kupambana na kuenea kwa virusi vya corona.

Taarifa ya KNVB ilisomeka: "Bodi ya soka la ushindani inafikiri kutoendelea na mashindano ya ligi kwa msimu wa 2019-20.

"Kutokana na uamuzi ya serikali, KNVB itawasiliana na Umoja wa mashirikisho ya vyama vya soka Ulaya, UEFA, na baada ya hapo uamuzi utachukuliwa.

"Ijumaa, klabu na wahusika wengine wa soka watakutaka kujadili matokeo yake na uamuzi utakaofikiwa."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# COSTA AFUNGUKA UBORA WA DYBALA

●●● Amtaja winga huyo ana kiwango bora zaidi ya mshambuliaji nyota wa Juventus Mreno...

**TURIN,** Italia

WINGA wa Juventus, Douglas Costa, amemtaja Paulo Dybala kama mchezaji hodari zaidi mbele ya mshambuliaji, Cristiano Ronaldo.

**Mchezaji huyo wa Timu ya Brazil alimchagua Dybala dhidi ya mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo wakati alipoulizwa na mashabiki 'live' kwenye mtandao wa kijamii wa Instagram.**

"Mchezaji mwenzagu hodari ni Paulino (Dybala)," alisema.

"Namchagua yeye kwa sababu namjua zaidi na nimecheza nae kwa kipindi kirefu na kwa kweli ni mtu mzuri zaidi," aliongeza kusema.

"Dybala ni mtu ambae ana aibu, lakini akiwa uwanjani anachotaka yeye kuisaidia timu kushinda, hivyo ukicheza nae unakuwa na wakati mzuri na hamasa kubwa kutoka kwake."

Costa amecheza pamoja na Dybala tangu alipojiunga kwa mara ya kwanza Juve kwa mkopo akitokea Bayern Munich mwaka 2017.

Ronaldo alihamia Turin mwaka mmoja baadaye katika uhamisho uligharimu kiasi cha euro milioni 112.

Costa kwa sasa anakaribia kurudi nchini Italia akitokea Brazil, ambako yupo kwenye mapumziko baada ya ligi Kuu Italia, Serie A, kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID 19).

Ligi hiyo ya Italia ilisimamishwa tangu Machi, mwaka huu kwa sababu ya mlipuko huo wa virusi vya corona na inatarajiwa timu zitaanza mazoezi Mei 4, mwaka huu.

Jumanne wiki hii, Serie A, ilitangaza kufikia makubaliano na klabu juu ya kumalizia msimu wa 2019-20, licha ya timu mbili za Torino na Sampdoria kupinga jambo hilo.

"Natumaini kurudi haraka nchini Italia," alisema Costa. "Nasubiri kwa hamu kubwa kurudi, kwa sababu, kwa sasa sijui nini cha kufanya hapa kwa kweli."

Juve walikuwa wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu kwa tofauti ya pointi moja na Lazio kileleni mwa Serie A huku mechi 12 zikisalia kumalizika kwa ligi hiyo.

## ZISIKUPITE

### COUTINHO AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA imekaribia kunasa saini ya kiungo wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho (27), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu ya Bayern Munich. ***(Sun)***

### WERNER ANUKIA ENGLAND

MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner, ameanza kujiandaa kuhamia katika Ligi Kuu England kwa kujifunza lugha ya Kingereza, huku Liverpool na Chelsea zote zinatajwa kuwania saini ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

### MANE KUONDOKA LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Sadio Mane (28), huenda akajiunga na Real Madrid baada ya kujisikia vibaya kutokana na Kocha Jurgen Klopp kutangaza alimpigia kura Virgil van Dijk katika kinyang'anyiro cha kuwania tuzo ya Ballon d'Or. ***(France Football - in French)***

### JORGINHO, CHELSEA KUTETA

WAKALA wa Jorginho ameweka wazi wanatarajia kufanya mazungumzo ya kusaini mkataba mpya na Chelsea baada ya kuwapo na tetesi za kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Italia anataka kuungana na kocha wake wa zamani, Maurizio Sarri, katika kikosi cha Juventus. ***(Calciomercato - in Italian)***

### WILLIAN KUBADILI UPEPO

KOCHA wa zamani wa Shakhtar Donetsk, Mircea Lucescu, amemtaka winga wa Chelsea, Willian (31), kukamilisha mchakato wa kuondoka katika klabu hiyo kipindi cha majira ya joto, tayari Juventus inatajwa ndio timu mpya atakayojiunga nayo. ***(Goal)***

### BALE KUBAKIA MADRID

REAL Madrid sasa inajipanga kumbakisha klabuni hapo Gareth Bale kwa msimu mwingine tena. Winga huyo wa Timu ya Taifa ya Wales, alionekana ana mpango wa kuondoka Madrid kwa sababu ya kutokuwa na maelewano na Kocha Zinedine Zidane. ***(Sun)***

### KARIUS KUREJEA LIVERPOOL

GOLIKIPA wa Liverpool, Loris Karius (26), huenda akarejea mapema Anfield akitokea Besiktas ya Uturuki baada ya kuwasilisha malalamiko Fifa, ya kutolipwa malimbikizo ya mishahara yake na klabu hiyo iliyomsajili kwa mkopo. ***(Evening Standard)***

### DIOP ATAKIWA SPURS

TOTTENHAM inajiandaa kumsajili, beki wa kati wa West Ham, Issa Diop (23), na straika wa Wolves na Timu ya Taifa ya Mexico, Raul Jimenez, ambaye ana umri wa miaka 28, kwa dau la pauni milioni 96.9 katika dirisha la usajili litakapofunguliwa. ***(Football365)***

### CITY YAMFUATA WHITE

MANCHESTER City imeweka wazi inamhitaji beki wa kati wa Brighton, Ben White, ambaye ana umri wa miaka 22 na yuko kwa mkataba wa mkopo kwenye klabu ya Leeds. ***(The Athletic, via Sports Illustrated)***

### BRUCE MAMBO MAGUMU

BEKI wa zamani wa Newcastle, Warren Barton, anafikiria mmiliki mpya wa timu hiyo maarufu Magpies atamfukuza Kocha, Steve Bruce na nafasi yake itachukuliwa na kocha wa zamani wa Spurs, Mauricio Pochettino. ***(Express)***

HABARI MICHEZO

# Waziri atamani kumfikia Kagere

**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI wa Mbao FC inayoshiriki Ligi Kuu, Waziri Junior, amesema yupo tayari kuendelea kupachika magoli mara baada ya ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakaporejea tena.

Waziri aliliambia gazeti hili jana, amefanya mazoezi vizuri na anaamini kiwango chake kimeimarika zaidi katika kipindi hiki cha mapumziko.

Mshambuliaji huyo alisema amefuata vema programu za mazoezi alizopewa na kocha wake na anawaahidi mashabiki wa Mbao FC kuona mambo mazuri.

"Nafanya mazoezi binafsi kwa wakati na kwa kufuata maelekezo, nitahakikisha ligi ikianza tena narudi na makali yangu ya kupachika magoli, ninajua ninawajibika kuibeba timu yangu, ila kuna timu zimenifuata, nimewaomba wafuate taratibu kwa sababu mkataba wangu na Mbao FC bado haujamalizika, ila nitaweka mbele maslahi," Waziri alisema.

Alisema yeye ni kiongozi wa familia hivyo analazimika kupambana kuhakikisha anapata fedha zitakazomsaidia kutimiza malengo yake.

# Nyota Azam FC kurejea dimbani

**Na Shufaa Lyimo**

MLINZI wa Kati wa Azam FC, Masoud Cabaye amesema hali yake imeimarika na anatarajia kuanza mazoezi kwa ajili ya kurejea kuitumikia timu yake katika mechi zilizosalia za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Cabaye alikuwa anasumbuliwa na maumivu ya nyama za japa katika mguu wa kulia, lakini sasa amepona na daktari amemruhusu kujiunga na wenzake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Cabaye alisema awali alitarajia kufanyiwa upasuaji, lakini baada ya maumivu yake kumalizika haraka, alibadilishiwa matibabu.

"Nashukuru sitafanyiwa upasuaji tena sehemu iliyokuwa inanisumbua, nimepona na nimebakiza wiki moja ili nianze mazoezi mepesi mepesi," alisema beki huyo.

Aliongeza kuwa ligi itakapoanza ataungana na wachezaji wenzake na anaamini kiwango chake kitakuwa kizuri.

"Timu ikianza mazoezi ya pamoja nami nitaungana nao, bado lengo langu ni kuipa mafanikio Azam FC ili tumalize msimu katika nafasi ya juu , ingawa haitakuwa kazi nyepesi," Cabaye alisema.



# NAMUNGO YAJIPANGA KUPAMBANA NA YANGA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Namungo FC ya Lindi umesema utahakikisha unafanya jitihada za kumbakiza mshambuliaji wake tegemeo, Reliants Lusajo ambaye anahusishwa na mipango ya kujiunga na Yanga.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa timu hiyo, Hassan Zidadu, alisema Namungo haiko tayari kumwachia mshambuliaji huyo kuondoka kirahisi ndani ya kikosi hicho.**

Zidadu alisema tayari walishaanza mazungumzo na Lusajo na yalifikia katika hatua nzuri kabla ya Ligi Kuu Tanzania Bara haijasimama ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Corona.

"Tulishafanya mazungumzo tangu awali, kabla ya corona na kumweleza nyota huyo bado tunahitaji huduma yake katika msimu unaokuja, hatutakuwa wanyonge katika hili, nadhani Yanga ni timu kubwa, hatuwezi kushindana nao, kikubwa kwetu tunafanya jitihada za kuhakikisha nyota huyo anaendelea kutusaidia katika msimu ujao," alisema Zidadu.

Alisema Kocha Mkuu wa timu yao, Thiery Hitimana, ameweka wazi hahitaji kufanya mabadiliko katika kikosi chake na alimtaja Lusajo kuwa ni mmoja wa wachezaji walioko katika mipango yake.

"Nadhani kwetu tunatapambana na Yanga kama kweli wanamhitaji, lakini pia mchezaji mwenyewe tunampa nafasi ya kumsikiliza kama ilivyo awali alitueleza bado hajafikiria kuondoka kwetu, akirejea kambini tunaendelea na mazungumzo naye," Zidadu alisema.

Aliongeza kuwa Lusajo ni mmoja wa wachezaji muhimu wa kikosi cha kwanza waliosaidia timu hiyo kufikisha malengo yake katika msimu wao wa kwanza wakishiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hadi Ligi Kuu inasimama, Lusajo alikuwa katika nafasi ya pili baada ya kufunga mabao 11 wakati kinara ni mshambuliaji wa Simba Mnyarwanda Meddie Kagere.



Wachezaji wa Fedha FC, wakifanya mazoezi ili kuimarisha viwango vyao kwenye Uwanja wa Hospitali ya Kivule jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# *Maxime azihofia timu vibonde Bara*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema 'kupanda na kushuka' kwa kikosi chake katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara kunasababishwa na ushindani uliopo kwenye mechi zote za ligi hiyo.

Maxime aliliambia gazeti hili jana msimu huu Ligi Kuu Tanzania Bara umekua mgumu zaidi kutokana na mabadiliko ya kanuni ambayo yamefanyika.

Beki huyo wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) na Mtibwa Sugar alisema kila timu ikiingia uwanjani inapambana kusaka ushindi ili kujiepusha na janga la kushuka daraja.

"Mechi zote zimekuwa ngumu, hasa ukicheza na timu zilizopanda, zinapambana katika kila mechi ili kujihakikishia nafasi ya kutoshuka daraja," alisema Maxime.

Kocha huyo alisema kikosi chake hakina tatizo na matokeo ya kushinda na kufungwa wanayopata yanatokana na ushindani uliopo kwenye ligi hiyo na si vinginevyo.

"Hakuna tatizo lolote ndani ya kikosi changu, ila tukubali msimu huu ligi ni ngumu sana, na ushindani ni mkubwa, hakuna mechi ndogo, tena ushindani unaongezeka unapocheza na timu ambazo zimepanda, zenyewe zinapambana ili zisishuke daraja," Maxime alisema.


Alisema kwa sasa anajitahidi kuwaeleza wachezaji wake kufuata maelekezo anayoyatoa kwa njia ya simu ili watakaporejea kikosini wake na kiwango imara.

Kagera Sugar ina pointi 41 baada ya kucheza mechi 29 na katika msimamo wa Ligi Kuu Bara iko kwenye nafasi ya nane wakati vinara ni Simba ya jijini Dar es Salaam.

# Michezo

Alhamisi Aprili 23, 2020

Nipashe

Costa afunguka ubora wa Dybala UKURASA 22




Ofisa Mtendaji Mkuu wa mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Senzo Mbatha. **PICHA : MAKTABA**

## Serikali yapunguza makocha wageni

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Harrison Mwakyembe, ametaka makocha wa kigeni wanaokuja nchini kuwa na wasaidizi wazawa badala ya kuja na makocha wengine kutoka nje.

Akihitimisha hoja zilizojadiliwa na wabunge wakati wa mjadala wa Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2020/21 jana jijini hapa, Mwakyembe, alisema kuja na makocha wasaidizi wa nje ni kuongeza gharama.

"Wasaidizi watafutiwe hapa hapa nchini, kocha kutoka nje anakuja na wasaidizi ni kuongeza gharama tu hasa kwenye hizi klabu zetu hili liangalieni sana,"alisema Mwakyembe.

Aidha, alisema kuna wasanii 1,934 ambapo serikali inafuatilia kwa kila msanii ni kiasi gani anatakiwa kulipwa kutokana na kazi zake.

"Kwa sasa tuna orodha ya wasanii 1,934 na tunafuatilia ni kiasi gani cha fedha wanatakiwa kulipwa hata waheshimiwa wabunge ambao ni wasanii pia tunawaona,"alisema.

Kuhusu kuongeza Bajeti ya Taasisi ya Sanaa Bagamoyo (Tasuba), alisema imeombewa Sh. million 250.

"Naamini Bunge lako litapitisha kwa ajili ya kuimarisha miundombinu na vifaa vya kufundisha," alisema.

Kuhusu idadi ya wachezaji wa kigeni watakaoruhusiwa katika Ligi Kuu Bara, Mwakyembe alisema ni jambo la kushangaza klabu za Simba, Yanga na Azam kununua wachezaji kutoka nje.

# Simba yajiweka mguu sawa

## ●●● Mabosi waendeleza mikakati ya ubingwa huku wakitamba wako tayari kumalizia...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI bado hatima ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa mwaka 2019/ 20 ikiwa haijajulikana, vinara wa ligi hiyo, Simba wameendelea kujiimarisha kila idara ili kuhakikisha wanatimiza malengo yao.

**Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mbatha, alisema wameendelea kufanya vikao vya mara kwa mara na benchi la ufundi ili kujiimarisha na kuwa tayari kumalizia msimu.**

Senzo, ambaye ni raia wa Afrika Kusini alisema pia wanahitaji kujiweka tayari na maandalizi ya msimu mpya licha ya kuwapo kwa hofu ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19).

Alisema ugonjwa huo umeleta changamoto katika kukamilisha majukumu yao mbalimbali, lakini wanalazimika kupambana ili kutoathiri shughuli na mipango ya klabu ya msimu huu ambao unaelekea ukingoni.

"Covid- 19 imebadilisha utendaji wetu wa kazi wa kila siku, hata namna ya kufanya vikao imekuwa ni changamoto, lakini lazima tutarejea katika maisha yetu ya mpira, tunatakiwa kuwa tayari," Senzo alisema.

Aliongeza Simba haitaacha kuendelea na mipango yake, ingawa kwa sasa wanafanya majukumu yao kwa njia nyingine.

"Tunaendelea na kazi kama kawaida, mipango yetu haiwezi kusimama, tunaendelea kupeana mwongozo na hatutaacha kuwajulisha wadau wetu kila tunachokifanya kuelekea mwishoni mwa msimu huu," aliongeza kiongozi huyo.

KUSHUSHA VIFAA

Katika kuonyesha wamedhamiria kusajili kikosi kitakachofanya vizuri kwenye msimu ujao wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba itasajili wachezaji wenye ubora kutoka ndani na nje ya Tanzania.

"Kama mlivyomuona Luis (Miquissone), basi chini yangu, Simba itaendelea kusajili wachezaji wenye viwango vya juu kwa sababu tunataka kupeperusha vizuri bendera ya klabu kwenye mashindano ya kimataifa, hilo ndio lengo kuu la klabu," alisema Senzo.

Aliongeza kwa kutumia mawakala mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, wamefanya mchakato wa usajili kwa umakini ambao utawapa matokeo chanya katika mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

Naye Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Crescentius Magori, aliliambia gazeti hili klabu hiyo inatakiwa kwanza kufikiria kufika hatua ya nane bora ya Ligi ya Mabingwa Afrika na baadaye ubingwa wa michuano hiyo.

"Utatakiwa kujihakikisha kuingia mara kwa mara katika makundi, halafu robo fainali, hapo tayari utakuwa unafikiria ubingwa wa Afrika, tunahitaji kuendelea kuwekeza, kwa kuanzia kuwa na wachezaji wenye uwezo wa kupambana kwenye hatua hizo za juu," Magori alisema.

Simba yenye pointi 71 ndio vinara wa Ligi Kuu Bara wakifuatiwa na Azam FC yenye pointi 54 wakiwa wamecheza mechi 28 huku Yanga iliyoko katika nafasi ya tatu ina pointi 51 lakini imeshuka dimbani mara 27.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >